

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 25 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatuhu)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni ya 33 fasili Ndogo ya (2) natoa taarifa kwamba leo majira ya 4.30 Mheshimiwa Sambi, Rais wa Jamhuri ya Comoro atakuja kulihutubia Bunge. Sasa hili hilo liwezekane namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu, Sera na Bunge) ili aweze kutoa hoja ya kuweza kumruhusu mgeni au wageni kutegemea Rais atakavyokuja, Rais wa Comoro basi aweze kuruhusu hawa wageni waingie ndani ya Bunge.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (URATIBU, SERA NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 150 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa hoja kwamba Bunge hatimaye baadaye liruhusu wageni watakaoandamana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Kiislam ya Comoro na wageni wake hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kabla sijawahoji niseme tu kwamba bahati mbaya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ana safari ya nje. Kwa hiyo, hataweza kumsindikiza mgeni wake. Kwa hiyo tunaowaombea ruhusa ni hao Rais mgeni yaani wa kutoka Jamhuri ya Kiislamu wa Comoro na ujumbe wake, hao ni ndio hoja iliyopo mbele yetu wawze kuingia ukumbini.

Kwa hiyo, wageni wataingia ukumbini, baada ya maswali nitaomba meza ya Katibu wakusaidieni kwa sababu mgeni wetu atazungumza lugha ya Kifaransa mtaona kuna vyombo hivi vimewekwa mbele yenu mtasaidiwa kuhusu matumizi yake ili tuweze kufuatalia vizuri hotuba hiyo, ahsante.

## **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali la kwanza kwa siku ya leo linaelekezwa Wizara ya Katiba na Sheria na linalizwa na Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 457

### **Ukarabati wa Nyumba za Hakimu za Mahakama**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati Serikali inajibu swali Na. 161 tarehe 14 Novemba, 2007 kuhusu kujenga nyumba za Mahakama na Majaji kulitolewa taarifa kuwa, miradi ya kufanya kazi hiyo inaanza kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu:-

Je, Serikali inasemaje juu ya kuzifanya ukarabati nyumba za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Mahakama zenyewe ambazo zimechakaa sana na nyingine hazifai kwa matumizi ya Binadamu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mahakama ya Tanzania inajenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo chini ya Mpango endelevu na ukarabati na ujenzi wa Mahakama hizo. Mpango huu ni wa miaka 5 ambao ulianza 2004/2005 utamalizika mwaka huu wa fedha. Ni sera ya Mahakama kuanzia sasa kwamba inapojenga au kukarabati Mahakama. Pia inajenga na kukarabati nyumba ya Hakimu. Jithada zinafanywa ili kujenga na kukarabati nyumba za Mahakimu kadri Bajeti itakavyoruhusu.

Hadi sasa Mahakama za Mwanzo 83 zimekarabatiwa na 28 zimejengwa chini ya utaratibu huu. Pia kuna Mahakama 8 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na Mahakama, na Mahakama 9 zinaendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi. Chini ya Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*LSRP*) Mahakama 3 za Mwanzo zinajengwa na Mahakama 4 zinakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Mahakama chini ya mpango endelevu inatarajia kukarabati Mahakama za Mwanzo 25 na kujenga majengo

mapya ya Mahakama za Mwanzo 5 na majengo matano mengine yataendelea kumaliziwa ujenzi wake chini ya Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (LSRP).

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na vile vile niipongeze Serikali kwa kujenga Mahakama mpya ya Mwanzo Mji mdogo wa Iguguno. Je, Serikali ilishakuwa tayari kujenga nyumba ya Hakimu pale Iguguno ambavyo imejengwa Mahakama mpya kwa sababu mpaka sasa hakuna nyumba.

Pili, katika mpango wa kukarabati hizi Mahakama na nyumba za Mahakimu. Je, atakumbuka kukarabati Mahakama za Kinyangiri, Iyambi, Nduguti, Kirumi na Ibaga zilizoko Iramba Mashariki?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumejenga Mahakama nzuri pale Iguguno na ni katika utaratibu huo huo tutajenga nyumba ya Hakimu katika Mahakama hiyo.

Kuhusu hizi Mahakama nne (4) ulizozitaja ni kweli tuna utaratibu wa kukarabati lakini kama nilivyosema inategemea bajeti. Kwa hiyo siwezi kumwahidi kwamba mwaka huu wa fedha tutafanya hivyo lakini kadri tutakavyo tunapata fedha tunakusudia kukarabati Mahakama hizo.

Na. 458

#### **Tatizo la Mirathi**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA (K.n.y. MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, mirathi ni tatizo kubwa na huchukua muda mrefu sana hadi warithi hukata tamaa kutokana na usumbufu:-

Kwa nini Serikali isiboreshe mfuko huo kama ilivyo kwa wastaafu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Ni kweli mirathi ni tatizo kubwa na huchukua muda mrefu warithi kukabidhiwa mirathi yao. Kimsingi Serikali haina mfuko maalum wa mirathi. Ni vema kufahamu kuwa mirathi ni mali iliyoachwa na Marehemu. Hata hivyo kimsingi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa taratibu za kugawa mirathi huchukua muda mrefu na sababu za msingi za ucheleweshwaji huo ni kama zifuatazo:-

- (a) Marehemu kutoacha wosia hivyo kusababisha mifarakano kati ya warithi na hata kati ya warithi na wasio warithi.
- (b) Mali za marehemu kuwa mbali na eneo analoishi msimamizi wa mirathi na hivyo kumwia vigumu kwa msimamizi wa mirathi kufuutilia mali hiso.
- (c) Kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu suala zima la mirathi kwa wananchi.

Wizara yangu immeanzisha mpango mahsusili ili kukabiliana na tatizo hili sugu. Mathalani Kitengo cha Wakala wa usajili Ufilisi na Udhagini (*RITA*) kimeanzisha utaratibu wa kutunza hati zote za Wosia ili kuwawezesha wananchi kuwa na mahali pa faragha na penye usalama wa kuhifadhi wosio. Kitengo hicho pia kitaanza kutoa elimu kuhusu masuala ya mirathi mijini na hata vijijini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa rai kwa wananchi kujenga tabia ya kuandika wosia mzuri na wa haki ili kuwaondolea watoto, wake zao na hata ndugu zao, waume zao usumbufu pindi wakati unapowadia.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inaendelea na zoezi zuri sana la kupeleka huduma na madaraka karibu na wananchi walipo. Naomba kujua kwa nini Serikali isikubali masuala ya mirathi yasiende mpaka kwenye Halmashauri ya Wilaya au kwa Mkuu wa Wilaya hasa kwa kujua kwamba mambo ya mirathi yanaanza kwenye Mahakama za Mwanzo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema masuala ya mirathi yanaanza kwenye Mahakama za Mwanzo na utaratibu huo ambao ameupendekeza kwamba tutumie Halmashauri ama Ofisi ya DC ni utaratibu ambao labda tuuchukue tuufanyie kazi tuone kama utasaidia kupunguza tatizo hili basi tutafanya hivyo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa kuna watumishi waliofariki miaka ya nyuma sana na wajane wao baada ya kupitia hatua zote za mirathi walileta vielelezo HAZINA ili waweze kulipwa haki aliyokuwa anastahili yule marehemu. Lakini ni muda mrefu na yaelekea kumbukumbu hiso zimepotea. Je, kwa kuwa hao wajane bado wapo tunaweza kufanya njia gani kuwasaidia ili wapate haki yao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, watumishi ambao wamefariki halafu mirathi yao ikawa haijalipwa kwa wasimamizi wa mirathi hiyo. Kwa

kweli utaratibu huo si mzuri lakini kinachotakiwa kwamba taratibu zifuatwe ili watumishi hao wajane au wasimamizi wa mirathi ile maana wasimamizi ndio wanaolipa sio lazima wawe wajane ila yule msimamizi ndio atakayelipwa halafu kisha yeye atawagawia wanaostahili kulipwa. Ningemshauri basi atuletee hilo Serikalini atupelekee Wizara ya Fedha ili tuone ni jinsi gani wajane au wale wanaostahili mirathi hii walipwe kwa sababu ni haki yao, wasimamizi wa mirathi kulipwa mirathi hiyo. (Makofi)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yetu ilishasaini mikataba ya huduma bora kwa wateja kwa kumaanisha kwamba Wizara itakuwa na utaratibu maalum kwa kutumia wakati maalum katika kutekeleza huduma zake kwa wananchi wa Tanzania. Na kwa kuwa eneo hili la mirathi limeonekana kabisa halitekelezeki kwa kuzingatia mikataba ile ya huduma bora kwa wateja. Je, Mheshimiwa Waziri atanieleza leo mikataba ile ya huduma bora kwa wateja ambayo Wizara yake pia ilishasaini na kuiridhia inaendaje sambamba na utoaji wa huduma ya upatikanaji wa mirathi kwa muda unaotakiwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Serikali wote tumetoa *clients chatter* ambazo zinaeleza kwamba itatolewa kwa muda gani huduma ile inayostahili.

Katika historia ya mirathi ni kwamba mirathi inapita katika sehemu nyingi si lazima ni Mahakama tu inaanza nyumbani ambako watu wanaohusika wanamchagua Msimamizi wa Mirathi kisha wenyewe wanakwenda wanamtangaza kwenye gazeti wanapeleka Mahakamani. Mahakamani napo hata wakishatoa kwamba fulani apewe kiasi fulani inabidi iende HAZINA. Kwa hiyo *clients chatter* zitawahusu watu wengi katika suala hili. Ninachoweza kusema katika Wizara ya Sheria bado hatujaweka clients *claims chatter* pale Mahakamani kuhusu kazi za Mahakimu. Na hili ni jambo la kulifiria kuanzia sasa. Wenzetu wa Kenya wanafikiria kuweka *clients service chatter* na Majaji kwamba Jaji atafanya kesi ngapi kwa mwaka. Kwa hiyo ni jambo zuri tunalifikiria na sisi tuone ni kiasi gani kwa sasa tuna *service chatter* za namna hiyo katika Mahakama za Mwanzo.

Na. 459

### **Samaki wa Mapambo Ziwa Nyasa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ziwa Nyasa lina Samaki wa mapambo wanaofaa kwa biashara ya Utalii:-

- (a) Je, kuna aina gani za Samaki hao na kwa uwingi ni kiasi gani?
- (b) Je, kuna leseni ngapi za uvuvi wa Samaki hao na wanavuliwa kwa kiasi gani?

(c) Je, Serikali inafaidika vipi na Samaki hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Professa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, samaki wanaovuliwa kwa ajili ya biashara ya samaki wa mapambo kutoka Ziwa Nyasa wamegawanyika katika makundi mawili makubwa kama ifuatavyo:-

·Kundi la kwanza ni samaki wale wanaoishi zaidi kwenye mawe au miamba amba ni aina (*species*) zipatazo 250 chini ya koo (*genera*) kumi. Baadhi ya koo muhimu ni “*Cyathochromis, Cynotilapia* na *Genyochromis*”.

·Kundi la pili ni samaki amba hawapendelei kuishi kwenye mawe na amba pia wengi wao hutumika kwa kitoweo na wako chini ya koo (*genera*) 38 zifuatazo. Baadhi ya koo kubwa ni *Alticorpus, Aristochromis, Nyassachromis* na *Aulonocara*”.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utafiti kubaini wingi ama idadi ya samaki wa mapambo katika Ziwa Nyasa kupitia Taasisi yake ya utafiti (*TAFIRI*). Taarifa ya utafiti huo zitatolewa kwa wananchi pindi matokeo yatakapopatikana.

(b)Mheshimiwa Spika, leseni za uvuvi wa samaki wa mapambo waliomo ndani ya Ziwa Nyasa hutolewa na Halmashauri za Wilaya husika kwenye eneo la maji ya ziwa hilo.

Kwa mfano, mwaka 2006 jumla ya leseni tano (5) za kuvua samaki wa mapambo zilitolewa. Kati ya hizo leseni nne (4) zilitolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, na leseni moja (1) ilitolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Mwaka 2007 leseni sita (6) zilitolewa na Halmashauri ya Wilaya Kyela na leseni mbili (2) zilitolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Kuanzia mwezi Januari hadi Mwezi Mei, 2008 jumla ya leseni sita (6) zimetolewa, kati ya hizo leseni nne (4) zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na leseni mbili (2) zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Idadi ya samaki wa mapambo waliovuliwa katika miaka hiyo ni kama ifuatavyo, mwaka 2006 samaki 12,661, mwaka 2007 samaki 10,403 na mwaka 2008 hadi mwezi Mei samaki 3,001 walivuliwa.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali inanufaika na samaki hao kutokana na wananchi wake kupata mapato ya mauzo ya samaki hao wa mapambo na Serikali yenyewe huingiza mapato yatokanayo na ada za leseni na ushuru wa kuuza nje ya nchi samaki hao. Kwa

mfano mwaka 2006 jumla ya samaki wa mapambo 12,661 wenyе thamani ya shilingi milioni 87 waliuzwa nje na Serikali ilikusanya ushuru wa shilingi milioni 6.5.

Vile vile mwaka 2007 samaki wa mapambo 10,403 wenyе thamani ya shilingi milioni 92 waliuzwa nje na Serikali ilikusanya ushuru wa shilingi milioni 5.3 Kwa mwaka huu hadi tarehe 30 Juni 2008, samaki wa mapambo 3,001 wenyе thamani ya shilingi milioni 36 waliuzwa nje na Serikali imekusanya ushuru wake shilingi milioni 1.5.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa uvuvi huu unafanywa zaidi na wageni sio Watanzania. Na kwa kuwa unafanywa bila usimamizi wa kutosha, nina maswali mawili. La kwanza Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uvuvi ili kuhakikisha kwamba unakuwa endelevu.

Swali la pili, kwa kuwa imeonyesha vile vile kwamba upande wa Ludewa pengine hawavui sana kwa hiyo haiwasaidii sana wananchi wa Ludewa. Lakini vile vile nahisi hata kwa upande wa Kyela na Mbinga wangeweza kuvua zaidi. Je, Serikali ina mkakati gani na utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba Serikali inafaidika zaidi na wananchi wa maeneo hayo wanafaidika na biashara ya samaki hawa wanahama?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Serikali katika uthibiti wa uvuaji samaki katika Lake Nyasa kwa sasa hivi Wizara yangu haisimamii. Lakini Halmashauri za Wilaya ndiyo zinasimamia uvuvi wa pale kuhakikisha kwamba hamna uvuvi wa haramu na uvuvi endelevu unafanyika. Lakini vile vile tumewahi kuwafundisha watu kule namna ya kuvua. Kwa hiyo, hilo Wizara inahusika.

Kuhusu Ludewa na Kyela kutovua ni kwamba kwa sasa hivi itahakikisha kwamba katika mwaka 2008/2009 tunajaribu kuweka kituo kule Kyela kuhakikisha kwamba uvuvi unaofanyika huko ni endelevu.

Na. 460

**Uanzishwaji wa Mashamba Madogo  
Madogo ya Pamba - Chunya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuanzisha mashamba madogo madogo ya kilimo cha Pamba – Chunya kama njia ya kukabiliana na Funza Wekundu (*red bowl worm*):-

- (a) Je, mashamba hayo yameanzishwa?
- (b) Je, ni lini hasa wananchi wa Chunya wataruhusiwa tena kulima zao la Pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesa, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika Wilaya ya Chunya mashamba ya majaribio yameanzishwa tangu msimu wa 2004/2005 katika vijihi vya Mapogoro, Mbala, Ifumbo, Magamba, Kanga, Galula na Chang'ombe.

Matokeo ya awali yalionyesha kwamba Funza Mwekundu (*Diparosic Castance*) ameonekana katika vijihi vyote hivyo isipokuwa Kijiji cha Mapogoro. Aidha, msimu wa mwaka 2005/2006 yameanzishwa majaribio ya kubaini madhara ya Funza Mwekundu katika vijihi hivyo, utafiti huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaruhusu kilimo cha pamba katika Wilaya ya Chunya na sehemu zingine za mikoa ya kusini pale itakapodhihirika kwamba mdudu huyu hayupo tena katika maeneo hayo. (*Makofi*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa mdudu huyu ameonekana hata kwenye nyasi na wala si kwenye pamba na kwenye majani mbalimbali. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuongeza utafiti zaidi juu ya mdudu huyu ili tumtokomeze na wananchi waruhusiwe kulima pamba?

Pili, kwa kuwa kitendo cha kuzuia kulima pamba kulipunguza kipato cha wananchi na Serikali iliahidi Bunge lako Tukufu kwamba itafanya utaratibu wa kuanzisha zao mbadala kwa wananchi hawa ambao waliathirika na zao hilo. Je, ni zao gani ambalo wananchi wamepewa kama zao la mbadala ili kuimarisha uchumi wao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba lazima tuendelee na utafiti wa kina kabisa kusudi hatimaye tuweze kumtokomeza mdudu huyu Funza Mwekundu.

Lakini niongeze kwamba kama alivyosema tuna mashamba kule Chunya ambayo yanafanyiwa majaribio sasa hivi kusudi tuweze kujua kwamba ni gharama kiasi gani ambazo zitamhitaji mkulima aweze kuzitumia ili aweze kulima pamba wakati huo huo mdudu huyu akiwepo. Matokeo haya yatatoka mwezi huu na nadhani mwezi ujao Septemba mwishoni tutakuwa tumeshapata matokeo haya.

Kuhusu zao mbadala nadhani hili ni suala la kukaa na kuangalia kwa sababu wananchi wenyewe wanajua ni mazao yapi yanaota vizuri na sisi wataalamu wetu wanajua ni mazao yapi yanaota vizuri hilo linaweza likazungumzika na tukaweza kujua ni mazao gani.

Lakini maeneo haya yana mazao yake. Maeneo ya Mbeya, Ruvuma yana mazao yake makuu. Maeneo ya Lindi yana mazao yake makuu kule ambayo ni korosho pamoja na kahawa, kwa hiyo mazao haya tungeweza kuyaendeleza zaidi wakati tunafikiria mazao mengine kama pamba. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na wenzetu wa Chunya kuomba kulima zao la pamba lakini bado hata mikoa tunayolima pamba baada ya kuhamasishwa na Serikali kwa kiasi kikubwa bei ya pamba iko chini sana, imeshuka kutoka shilingi 700/= mpaka shilingi 400/= kwa kilo. Nadhani Mkoa wa Singida na Manyara.

Je, Serikali iko tayari kutazama upya bei ya pamba ili kuwatia moyo wananchi wanaolima pamba waendeele kulima pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa jumla Serikali haipangi bei za pamba ama bei ya zao lolote kwa sababu ilishajitoa. Bodi ya kupanga ilishajitoa kwenye shughuli hiyo. Bei hupangwa kutokana na *World Price* yaani bei ya soko la dunia na *demand*.

Kama mahitaji ni makubwa basi bei itapanda na mahitaji yakishuka na kama kuna *high production* maana yake bei nayo itashuka.

Lakini ninachomshauri Mheshimiwa ni kwamba tuhamasishe wakulima wetu wajiunge kwenye Vyama vyta Ushirika kusudi vyama vile viweze kuwasaidia kudai bei nzuri zaidi. (*Makofi*)

Na. 461

#### **Nyambiti Ginnery Kutekelezwa na Ushirika wa Nyanza**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nyambiti *Ginnery* iliyopo katika kijiji cha Mwabilanda imetekelezwa na Ushirika wa Nyanza na mabati ya majengo hayo yameanguka chini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isitoe kibali kwa wananchi wanaoishi eneo hili wauziwe mabati hayo?

(b) Je, kwa nini Ushirika wa Nyanza haufuatilii mali zake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (*NCU*) kinamili kiinu cha kuchambulia pamba cha Nyambiti kilichopo katika kijiji cha Mwabilanda. Kinu hicho kina miundo mbinu mbalimbali yakiwemo maghala 15 pamoja na mitambo ya kukamulia mafuta ambayo ni ya miaka mingi. Kutokana na uchakavu wa miundombinu yake, baadhi ya maghala hususan yale yaliyojengwa kwa kutumia mabati huweza kuezuliwa na upopo mara kwa mara. Kampuni ya Igunga *Cotton Company* ambayo imeyakodi maghala hayo imekwishaanza kuyafanya ukarabati maghala yaliyoezuliwa mabati ili yaweze kutumika katika msimu huu wa pamba unaoendelea. Hii ni pamoja na kununua vipuli na kukarabati vinu vya kuchambulia mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kutoa kibali cha kuuzwa kwa mali za wanaushirika kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anapendekeza, bila wao wenywewe kupanga na kuamua hivyo kuitia katika mikutano yao mikuu ya wanachama. Lakini kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameguswa na hali ya mali za wanaushirika, Serikali nayo pia inahimiza utunzaji wa mali za Vyama vya Ushirika na itaendelea kuhimiza vyama vyote vya ushirika kikiwemo hiki cha Nyanza kusimamia vizuri mali zao ili ziweze kuleta manufaa kwa wanaushirika na wananchi wote kwa ujumla.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza suala dogo tu. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini imenishtusha kwamba kumbe kuna mwekezaji ambaye tayari amepatikana pale lakini wananchi wa eneo hilo hawafahamu. Je, Serikali sasa inaweza kwenda pale mahali wakawajulisha wananchi juu ya mwekezaji huyo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa wananchi wa eneo hilo hawajaambiwa kwamba kuna mwekezaji.

Je, huyo mwekezaji hawezo sasa kuja kuanza kufanya usafi wa eneo hilo kwa sababu majani yamejaa sana pale, akaanza kwanza uwekezaji ili wananchi wajue kuna mtu yuko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa ujumla niseme kwamba kazi ya kuwajulisha wananchi kuhusu mwekezaji huyu ambaye amepata mkataba wa miezi minne kuanzia tarehe 1 Julai mpaka tarehe 31Oktoba, 2008 ni kazi ya chama au viongozi wa Chama cha Ushirika cha Nyanza. Kwa hiyo, nawashauri viongozi wa Chama cha ushirika cha Nyanza, waende kwa wananchi wawajulishe kwamba maghala hayo sasa yameshakodishwa kwa Kampuni ya *Igunga Cotton Company*.

Pili, mwekezaji huyu nadhani ananisikia, tunamshauri afanye usafi na aishi vizuri na wananchi wanaokaa eneo lile kusudi wananchi waweze kujua kwamba wamepata mwekezaji ambaye pia anaboresha mazingira ya eneo lile.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa Waziri amezungumzia suala la Vyama vya Ushirika; na kwa kuwa vyama vingi vya ushirika vina matatizo mengi sana na Serikali inawajibu kwa sababu imechaguliwa na wananchi. Kwa vile Nyanza ina mali nyingi ambazo sasa hivi zina utata mwangi. Je, Serikali inatoa tamko gani ili kuwanusuru wananchi wanaushirika wa Nyanza kutokana na mali hizi kuendelea kutumika vibaya zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi ipo Kamati ambayo inashughulikia mali hizi za vyama vya ushirika hasa hiki cha Nyanza na vilevile Mkuu wa Mkoa wa Nyanza pia anashughulia suala hili kwa undani kabisa. Kwa hiyo, jibu hili linahitaji litolewe vizuri. Kwa hiyo nadhani tukionana na Mheshimiwa Mbunge baadaye nadhani nitampa majibu ambayo baada ya kuwasiliana na wenzangu kwamba wamefikia hatua gani ili mali hizi za Nyanza ziweze kunusurika.

Na. 462

#### **Vituo vya Kukuza Michezo**

**MHE. NURU A. BAFADHILI (K.n.y. MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hapa nchini kumeanzishwa vituo mbalimbali binafsi vinavyohusisha na kukuza na kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu kama vile Makongo Sekondari, *Pangolin football Academy, YOC Elite Youths Sports Academy, Morogoro Sports Academy* na kadhalika.

Kwa kuwa, vituo hivyo bado ni vichanga na vinahitaji msukumu ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi; Je, Serikali inachukua hatua gani za ziada kuvisaidia vituo hivyo katika kutunza na kutimiza malengo hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika nyakati tofauti imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za ziada kuksaidia Maendeleo ya michezo hapa nchini ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa Baraza la Michezo nchini (BMT), Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Vilabu na Taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na Maendeleo ya Michezo mbalimbali ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu.

Kufuatia kuanzishwa kwa vituo mbalimbali binafsi vinavyojishughulisha na kukuza na kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu kama alivyovitaja Mheshimiwa

Mbunge, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa ili kuvisaidia vituo hivyo katika kutunza na kutimiza malengo yake.

Hatua ya msingi kabisa ni pamoja na kuviagiza vituo hivyo kuptitia vyombo nilivyovitaja kuhakikisha kuwa, masharti na taratibu za kuanzisha zimefuatwa, kuandaa ratiba ya mafunzo ya mashindano mbalimbali nadharia na vitendo, ili vijana wanaojiunga wapate uzoefu na mbinu mbalimbali za kimichezo na hivyo kuweza kujijengea uwezo wa kucheza na kushiriki mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa waanzilishi au wamiliki wa vituo vya michezo kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinaanzishwa kwa kuzingatia vigezo vinavyotambulika kitaifa na kimataifa na sio ili mradi wanawakusanya watoto kwenye vituo bila kutimiza mahitaji yake.

Aidha, natoa wito pia kwa Waheshimiwa Wabunge, wafadhili mbalimbali na wadau wa michezo kwa ujumla kushirikiana na Viongozi wa Vituo vya Kuendeleza michezo vinavyoanzishwa kwa kutoa msaada pale unapohitajika kwa lengo la kuibua vipaji vipya, kukuza na kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali inatilia mkazo sana katika michezo na kwa kuwa kuna viwanja vingi vinatolewa na kuruhusu watu kujenga nyumba zao na watoto kucheza barabarani kitu ambacho kinawasababishia ajali nyingi. Je, Serikali inatumbia nini kuhusu hilo?

Swali la Pili, kwa kuwa wanamichezo wetu waliotuwakilisha katika Michezo ya Olimpiki nchini China hawakupata hata medali moja. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu aibu hii iliyotupata na itatusiadida lini kuweza kutujengea shule ambazo zitakuwa shule maalum za michezo zitakazoandaa wanamichezo watakaoweza kuiwakilisha vizuri nchi yetu? Ahsante (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bafadhili kama ifuatavyo:-

Kuhusu viwanja ambavyo vinatumwa kwa kujengwa majengo mbalimbali, ni makosa kwa viwanja vile ambavyo vimewekwa kwa ajili ya michezo mbalimbali. Natoa wito kwa Halmashauri mbalimbali za nchi yetu kuhakikisha kwamba kunakuwepo na viwanja vya kutosha kwa ajili michezo mbalimbali ili vijana wetu wapate nafasi ya kukuza vipaji vyao.

Kuhusu mambo yaliyotokea kule China, mambo yaliyotokea kule China mimi nafikiri kwamba si aibu kwa sababu watu wameenda kule kushindana kule na kila mmoja amejiandaa vya kutosha ili ashinde. La msingi ni sisi wenyewe kujiimarisha ili kwa siku zijazo tupate medali za kutosha kwa ajili ya nchi yetu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Slaa swali la nyongeza. Nyie watu wa Manyara nyie ndiyo mlitakiwa mtupatia hawa watu hawa. Sijui kwanini...(Kicheko)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha unajulikana hasa kwa michezo ya riadha mbio ndefu; na kwa kuwa utafiti unaonyesha sana kwamba nchi zinazoshinda ni zile zilizomakini na zile zinazofanya maandalizi mapema na zinazofanya maandalizi; na kwa kuwa kama tulivyosikia jana Uingereza imekabidhiwa *torch* kwa ajili ya mashindano ya mwaka 2012 ili waanze maandalizi mapema.

Waziri yupo tayari sasa kulieleza Bunge hili mpango mkakati ambapo utahakikisha kwamba wachezaji wetu wa nyanja zote wanaandaliwa kikamilifu na Bunge linafuatilia *progress* yake ili kuondokana na hii aibu ambayo wachezaji wetu wanaitwa wasindikizaji na watalii?(Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Slaa kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kabisa kwamba kuna haja ya Serikali na Bunge kujua mkakati maalum inaandaliwa kwa ajili ya kujenga wanariadha wetu ili kuleta heshima kwa michezo ijayo hasa ya Jumuiya ya Madola na Olympic ijayo kule London. Nafikiri juzi mmesikia hapa Mheshimiwa Rais mwenyewe ameonyesha mfano kwa kuahidi kwamba atasaidia kuajiri kocha wa riadha ili kuimarisha michezo hapa nchini.

**MHE. MARTHA UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa sambamba na kukuza vipaji vya vijana katika mchezo wa mpira wa miguu; na kwa kuwa Serikali sasa hivi inaelekeza nguvu katika kukuza vipaji vya vijana wetu katika mchezo wa riadha; na kwa kuwa Mkoa wa Manyara unaonyesha kuwa na vijana wengi wenye vipaji hivyo. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba ni vizuri sasa na ni wakati muafaka kujenga *centre* kubwa kwa ajili ya michezo hii ya riadha Mkoani Manyara na kwa kuwa hali ya hewa pia inaruhusu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tungependa sana Serikali ijenje centre katika Mkoa wa Manyara, lakini Serikali imejitoa katika masuala haya. Kwa hiyo, nawaomba wananchi wenyewe na viongozi wa Mkoa wa Manyara wajikusanye ili kuomba watu mbalimbali kujenga *centre* kwa ajili ya maslahi ya Mkoa wa Manyara.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa nchi zote zilizofanya vizuri au karibu zote zilizofanya vizuri ni Serikali zao zimejenga vyuo vya michezo. Mimi sioni

kwanini Serikali yetu iseme inajitoa kwenye jambo la michezo ambalo si biashara bali ni heshima ya nchi. Kwanini Serikali yetu isijenge chuo badala ya kusema kuwa inajitoa? Michezo si biashara. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mimi jana niliposikia wakimbiasi wetu wa Marathon mmoja aliugua ghafla kabla ya kukimbia na mwingine aliyeshinda sana akawa wa 50. Ahh kweli (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)**  
**(K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Malecela, kama ifuatavyo:-

Nasema hatuwezi kujenga Chuo katika kila Mkoa kwa sababu ni gharama kubwa sana. Lakini Serikali inacho Chuo cha Michezo kule Malya, cha kisasa kabisa. Napenda Waheshimiwa Wabunge waende wakaangalie jinsi Serikali ilivyowekeza vya kutosha katika chuo kile kwa ajili ya maslahi ya taifa letu. Hatuwezi kujenga chuo kwa kila Mkoa.

Hata hivi vyuo tulivyo navyo vya *Academy* vimesaidia sana kukuza mpira wa miguu hapa nchini na michezo mingine. Kwa mfano wachezaji wetu wa mpira wa miguu kwa ngazi ya taifa wengi wao wametokana na vyuo kama hivi. Kwa hiyo, si lazima Serikali iwekeze. Kwa mfano tunaye Bwana John Tegete amesoma *Makongo High School*, huyu ni mchezaji wa Yanga na anacheza Timu ya Taifa, kuna Kigi Makasi kasoma *Rolling Stone* wa Yanga anachezea *Taifa Stars*, kuna Amir Maftah, *Rolling stone* wa Yanga *Taifa Stars*.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri wachezaji ni wa Yanga tu? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)**  
**(K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, Adam Kingwande wa *Jitegemee Secondary* wa *Simba Taifa Stars*, *Meshack Abel Rolling Stone* wa Simba Taifa. Kwa hiyo wapo wengi ambao wametokana na *academy* kama hizi. (*Kicheko*)

Pia hivi karibuni tunatarajia kupeleka vijana sita ambao wapo kwenye *Tanzania Soccer Academy* ya *TFF* nchini Uingereza kwa ajili majoribio. Kwa hiyo, hoja si Serikali iingilie, hata watu binafsi wanaweza kuwekeza na kuendeleza michezo hapa nchini kwetu.

Na. 463

**Fedha za Kodi ya Majengo Kupeleka kwenye Halmashauri**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge la Tanzania limekwisha pitisha Muswada wa Sheria ya Kuruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kuzisaidia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kukusanya kodi ya majengo (*Property Tax*).

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa fedha za kodi ya majengo zinazokusanywa na *TRA* zipelekwe moja kwa moja katika Halmashauri husika badala ya kupitia Hazina?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi wa April, 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kuruhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania kuzisaidia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kukusanya kodi ya majengo (*Property Tax*) Muswada huo ulieleza wazi kuwa zoezi hili litaanza mwezi wa Julai, 2008 kwa kipindi kisichozidi miaka mitano. Fedha zitakazokusanywa hazitapita Hazina zitapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika. Fedha zote za kodi ya majengo zitakusanywa kupitia akaunti moja ya *NMB* kwa jina la Kamishna wa Kodi za Ndani kwa ajili ya Halmashauri na baadaye zitahamishiwa kwenye akaunti za Halmashauri husika ndani ya kipindi kitakachokubalika na Halmashauri hiyo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabla sijaauliza swalii naomba niishukuru na kuipongeza sana *SIDO* kwa kukubali kuwakopesha Wajasiliamali zaidi ya 100 wa Wilaya ya Mpwapwa. Sasa swalii; kwa kuwa uthamini wa majengo mengi ya Halmashauri za Wilaya, miji, Manispaa na Majiji ulifanyika miaka mingi iliyopita na hawajafanya tathimini ya majengo haya kwa muda mrefu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa iko haja ya kufanya uthamini upya ili fedha zitakazokusanywa ziwe za kutosha kwa ajili Halmashauri zetu za Wilaya?

Swali la pili, kwa kuwa *TRA* wanafanya kazi nzuri sana na wanauzoefu mkubwa sana wa kukusanya mapato. Je, kwa kuwa zoezi hili linaanza Mkoa wa Dar es Salaam. Je, Mikoa mingine Serikali imeweka mkakati gani kuhusu kukusanya mapato haya ya kodi ya majengo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):**  
Mheshimiwa Spika, ni kweli tunaanza kazi hii kwa Mkoa wa Dar es Salaam na ni kweli kwamba uthamini wa majengo mengi katika Mkoa wa Dar es Salaam umefanyika mwaka 2000. Hata hivyo kodi ambayo imeKwa maana hiyo wazo la Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa. Kuna haja tathimini mpya na nataka nimweleze kwamba hivi sasa Wizara

yangu, *TRA* kwa kushirikiana na TAMISEMI wameshaanza mazungumzo na jinsi ya kufanya tathimini mpya kwa majengo yaliyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu la swali lake la pili, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mamlaka ya kuamuru Mikoa mingine ianze kazi kama hii yapo chini ya Waziri wa TAMISEMI kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo Waziri wa TAMISEMI atakapotoa katika gazeti kwamba Mkoa moja au Mikoa ianze shughuli hii basi sisi kama watendaji ndani ya *TRA* tutakwenda kufanya kazi hiyo wakati wowote ambapo Waziri wa TAMISEMI atakapo tangaza kwenye gazeti.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kwa kweli *TRA* inafanya kazi nzuri sana hapa nchini kwa kukusanya mapato; na kwa kuwa Halmashauri nyingi zinashindwa kukusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali kwa kukosa wataalam. Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati kwa *TRA* kukusanya kodi zote halafu ipeleke kwenye Halmashauri za Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimweleze Mheshimiwa Msindai kwamba jukumu la kukusanya kodi za Halmashauri liko chini ya Halmashauri yenewe. Sisi kama *TRA* ni kuwasaidia tu ili kuongeza uwezo wao wa kukusanya mapato. La msingi hapa ni kuzipatia utaalam zaidi Halmashauri zetu ili ziweze kukusanya mapato. Kwa hiyo, *TRA* iko tayari kuwasaidia kuwapatia utaalam na iko tayari kuwafunza watendaji wa Halmashauri ili waweze kutekeleza majukumu hayo.

Na. 464

#### **Maafa Yaliyotokana na Wakimbizi Wilayani (Ngara)**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (K.n.y. MHE. PROF. FEEDHAM F. BANYIKWA) aliuliza:-**

Kwa kuwa, kuwepo kwa wakimbizi Wilayani Ngara kumeleta ongezeko la uhalifu hasa mauaji ya wananchi:-

(a)Je, ni wakazi wangapi wamepigwa risasi na kuuawa kati ya wmaka 1994 – 2000 Wilayani Ngara?

(b)Je, ni majambazi mangapi walikamatwa kwa kuhuka na uvunjaji wa Sheria na mauaji katika kipindi hicho?

(c)Je, Serikali itatoa fidia gani kwa wale walipoteza maisha kutokana na vifo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBOYA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feedham F. Banyikwa, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 1994 – 2000 katika Wilaya ya Ngara Mkoani Kagera, wakazi waliopigwa risasi na kuuawa ni 47. Majambazi waliokamatwa kwa kuhusika na uvunjaji wa Sheria na mauaji katika kipindi hicho ni 21.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina utaratibu wa kulipa fidia mhanga au ndugu wa mhanga aliyekuawa au kujeruhiwa katika matukio ya uhalifu hasa ujambazi. Hata hivyo, kwa yale matukio ambayo watuhumiwa wa uhalifu watafikishwa Mahakamani, Mahakama pamoja na kutoa adhabu inaweza pia kumtaka mtuhumiwa aliyepatikana na hatia kulipa fidia kwa mhanga wa tukio hilo la uhalifu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa *Operation* nyingi zimefanyika katika Mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa maeneo ambayo yameathirika na wakimbizi ili kunyang'anya bunduki ili kupunguza uhalifu na haujapungua. Je, si vema Serikali ikarudia *operation* hii ili kuweza kupunguza bundiki zinazotumika katika kuwavamia wananchi na kuwaua katika Mikoa hii?

Swali la pili, Mikoa hii imeathirika sana kimazingira na mara nyingi wananchi wamekuwa wakidai fidia na hata mwuliza swali la msingi alikuwa anazungumza kuhusu fidia ya watu waliouawa; na mikoa hii imeshaombwa ilipwe fidia na *UNHCR*. Je, ni lini Wizara hii itasaidia ili Mkoa wa Rukwa, Kigoma na Mkoa wa Kagera kwa pamoja ifidiwe inavyostahili kutokana na uharibifu wa mazingira na watu wake ambao wameuawa kwa kuwaweka wakimbizi katika Mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kwanza la kurudia *operation* nasema kwamba hilo nimelipokea na tutalijadili na kutizama nini tutafanya lakini ni jitihada ambazo tulizonazo ndani ya Wizara na vyombo husika ili kuhakikisha kwamba matatizo ya hawa majambazi katika maeneo haya yanatokomezwa na yanakomeshwa lakini hilo nalichukua.

Kuhusu la pili, niseme tu kwamba iko tofauti kati ya kutoa fidia kwa wananchi wote husika na pia kutoka fidia katika familia ambazo watu wameathirika ama wameuawa na majambazi na nasema hivi ni Sera ya Serikali na sio ya Tanzania tu lakini popote duniani huwezi ukasema kwamba Serikali inaweza ikafidia wananchi wote ambao wamepata matatizo kutokana na majambazi kwa hiyo wapate fidia.

Ziko sheria na taratibu na tutakwenda hivyo lakini kuhusu suala la mazingira napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni suala ambalo tunazungumza na watu *UNHCR* wakati hii programu ya kuwarejesha wakimbizi kurudi makwao inakwenda awamu kwa awamu na tutatizama jinsi tunavyoweza kufaidika. Kwa kweli tunajitahidi na

naweza kusema wazi kwamba Serikali imejitahidi kadri iwezavyo kuwabana *UNHCR* na kuwabana *International Community* waweze kutambua mchango ambao Tanzania imeuweka katika masuala ya kupokea wakimbizi duniani.

**MHE. DANIEL N. NSAZUNGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri amesema Serikali haina mpango wa fidia kwa wahanga waliouliwa sio na ujambazi, waliouliwa na wakimbizi. Sasa, Serikali haioni wakati umefika ianzishe mchakato na wenzetu wa *UNHCR* kufidia wahanga walioathirika na wakimbizi sio majambazi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi linasema wahanga waliouliwa na majambazi sio na wakimbizi na mimi nimejibu katika mithili hiyo. Lakini kwa kuwa anazungumzia wale waliouawa na wakimbizi naomba nikiri kwamba hilo ni swali jipya ambalo tutalichukua na kulitazama ndani ya Wizara yetu na kwa kweli siwezi kulitolea jibu hapa sasa hivi.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hapa ameeleza kwamba wananchi 47 wameuawa katika Wilaya ya Ngara peke yake lakini idadi hii inazidi kuongezeka ukijumuisha Wilaya nyingine za Mkoa wa Kagera; na kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani inaonyesha kwamba imemewa katika kupambana na majambazi haya. Je, ni kwanini Wizara hii isiombe Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kuwasaidia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, abadani sitakiri kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi imeshindwa. Maana yake si kweli. Tunalozungumzia ni kwamba ukitizama idadi ya matukio ambayo yamekuwepo nchini na ukatizama jinsi Serikali imekuwa ikitabili na tatizo hili kwa kweli tutakubaliana kwamba jitihada kubwa zimekuwa zinafanyika na kweli zitazidi kufanyika. Tatizo ambalo tumekuwa nalo ni kwamba na hili swali limekuwa likijirudia rudia kwenye Bunge lako hili ni kwamba *tactics* na njia na taratibu ambazo hawa majambazi wamekuwa wanatumia zimekuwa zinabadilika wakati kwa wakati.

Kwa hiyo, inabidi *response* ya Serikali pia ibadilike kufuatana na mazingira ambavyo yanabadilika. Lakini napenda kusema kwamba hatujalemewa na tunaendelea kupambana na majambazi na *operation* zipo mbalimbali na iko *operation* kubwa ambayo Kamanda Tossi amekuwa anaelekeza katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba Serikali bado haijalemewa na Wizara yangu bado haijalemewa na tunaendelea; ni kiasi cha kuweza kupata nyenzo za kisasa na vifaa vya kutosha kiasi cha kuiwezesha Wizara iweze kukabiliana na hali halisi.

Na.465

#### **Msongamano wa Wafungwa Kwenye Gereza la Babati**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa Magereza ni mahali pa kurekebisha watu waliolikosea Taifa kwa muda, hivyo huduma zinazozingatia haki za binadamu ni lazima ziwepo:-

- (a) Je, Serikali ni mpango gani wa kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu kwenye Gereza la Babati wanaotoka Wilaya za Hannang na Simanjiro ambazo hazina Magereza?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati Gereza la Babati hasa sehemu ya wazi inayotumika kama bwalo na pia kuweka magodoro mapya na kutoa yale yaliyochakaa?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo la msongamano katika Gereza la Babati, mnamo mwezi Januari, 2008, Halmashauri ya Wilaya ya Hannang imetupatia eneo la ekari 395 ambalo lilikuwa linamilikiwa na *NAFCO* pamoja na miundombinu yake.

Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 tayari Serikali imeshapeleka jumla ya Tsh. 26,444,440/= ili kukarabati mojawapo ya majengo yaliyopo ili litumike na mafundi na wafungwa watakaokuwa wakifanya kazi za ujenzi wa Gereza hilo jipya la Hannang. Bweni la awali litakalojengwa litakuwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa 50. Hivyo mahabusu toka Wilaya ya Hannang watakuwa wanahifadhiwa katika Gereza hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kuhakikisha kwamba Magereza yote hapa nchini yanakuwa na huduma muhimu na za kuridhisha kwa wafungwa na mahabusu, nia hiyo nzuri ya Serikali inashindwa kutimia kutohana na uhaba wa bajeti. Hata hivyo, Serikali yetu inaheshimu haki za binadamu, hivyo kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu, ukarabati wa kina utafanyika katika Gereza la Babati ikiwemo kubadili magodoro ya wafungwa ambayo ni kweli kwa sasa yamechakaa.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi kuna utaratibu mzuri ambao Wizara imefanya kupeleka mahabusu kwenda kusikiliza kesi zao kwa kutumia usafiri wa mabasi; Je, utaratibu huo sasa kule Mikoani Mheshimiwa Waziri anasema nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani hapa katika Bunge hili Tukufu, alieleza kwamba huo ni mpango ambao tumeanza na tumeanza katika Mikoa kadhaa na tutakwenda hivyo hivyo jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha ili tuhakikishe kwamba hii programu inakuwa ni ya nchi nzima, siyo ya sehemu maalum. Lakini,

tutakwenda kadiri tutakavyokuwa tunapata fedha na shabaha na lengo ni kuhakikisha kwamba inakuwa ni programu ya nchi nzima. Ahsante sana!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali sasa umefika ukomo, naona tumalize swali la mwisho la Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Na. 466

### **Ujenzi wa Soko Eneo la Kipulapula**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Wakati Wizara ya Miundombinu inajenga barabara kati ya Lupembe (Njombe) na Taweta (Kilombero):-

Je, kwa nini Serikali isijenge soko eneo la Kipulapula lililopo katikati ya Taweta na Madete (Lupembe) ili kupunguza matatizo ya uuzaji wa mazao ya wakulima wa Taweta na Tanganyika (Kilombero) na Lupembe (Njombe)?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Makwetta kuwa ujenzi wa soko katika eneo la Kipulapula lililopo katikati ya Taweta na Madete utapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya uuzaji wa mazao ya wakulima wa Taweta, Tanganyika na Lupembe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingependa sana kuona kwamba kuna masoko likiwemo soko katika eneo la Kipulapula, yatakayorahisisha biashara na hivyo kuwasaidia wananchi kuinua vipato vyao na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Rais, Mungu ibariki Comoro, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa mapokezi haya ya ukumbini kwa mgeni wetu. Niongezee tu kutangaza kwamba ule Mkutano wa Kamati ya Uongozi sasa tena itabidi uahirishwe kwa sababu tunaendelea tena na mgeni wetu hadi saa 9.00 kwa hafla ya chakula cha mchana pale St. Gasper.

Kwa hiyo, haitawezekani kukatiza hapa katikati na kufanya mambo mengine. Tutatangaza kesho asubuhi muda muafaka wa mukutano huo. Kwa kuitikia wito wa ushirikiano wa Mheshimiwa Rais wa Comoro, napenda kwa niaba yenu, nitoe mwaliko rasmi na sasa Spika wa Comoro, anasikia kwamba yeze na Wabunge idadi ambayo wanaona inafaa tutafurahi sana kuwapokea hapa mwezi Novemba, 2008 tutakapokuwa hapa tena. Muda huo ni mzuri tu, kwanza mwezi wa Ramadhani utakuwa umeshapita na hata wale wanaofunga sita zitakuwa zimekwisha. Kwa hiyo, tutaomba sana mje. Ninayo sababu ya kuwaomba mje haraka kiasi hicho kwa sababu ninyi mkija tu mwezi wa Novemba, 2008 nakusudia kabla ya mwisho wa mwaka, sisi tuje Comoro. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 05.51 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, poleni kwa kazi nzito ya leo kipindi cha asubuhi. Nafahamu wote tulikuwa na ugeni mkubwa wa rafiki yetu, jirani yetu na nadhani wananchi walishuhudia yale matukio yaliyotoka leo asubuhi katika Ukumbi wetu, basi baada ya kumaliza shughuli ile asubuhi, naomba nichukue nafasi hii sasa niwakaribishe ili tuweze kuendelea na ajenda za leo na tutaendelea na hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi na jioni hii ya leo tutaendelea na wachangiaji ambao wamekuwa wakijiandaa kwa ajili ya kuendelea kuchangia hoja hii. (*Makofi*)

Lakini Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu na mimi nichukue nafasi hii niwape pole sana wapiga kura wangu wa Kijiji cha Luhimba na wengine wote ambao wamepata maafa makubwa nyumba zao takribani kumi zimechomwa moto huko. Kwa hiyo, naomba wawe na subira na mimi nitaungana nao baada ya muda si mrefu.

Baada ya kusema hayo sasa naomba nimwite Katibu ili atuongoze kwa shughuli ya jioni ya leo. Katibu! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na kadri ya orodha yangu naomba niwatamke wachangiaji wa tano wa mwanzo na kama bado hawajaingia hapa Ukumbini basi waweze kujiandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Estherina Kilasi, atafuata na Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Magale John Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba na Msemaji wa tano atakuwa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. (*Makofi*)

Kwa hiyo, baada ya kuwataja wachangiaji hao watano wa mwanzo naomba sasa nimwite Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali ili aweze kuanza kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Kilasi. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Nikushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mtu wa kwanza jioni ya leo kuchangia hoja hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Lakini kabla sijaanza niungane na wewe kuwapa pole wapiga kura wa jimbo lako kwa yote ambayo yamewakuta na sisi tunaungana na wewe kuwapa pole. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kwanza kwa hotuba yao nzuri, fupi, yenye kueleweka. Lakini nikaona sio ajabu kwa sababu walioandika wote ni Wahasibu, Wahasibu hawana maneno mengi, wanaenda moja kwa moja kwenye hoja inayozungumziwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ya kuchangia. Wenzetu wametoa nini ambacho wanategemea kufanya katika mwaka huu wa fedha unaoanza 2008 kuishia Juni, 2009. Napongeza kwa yote ambayo wameyaweka vizuri. Lakini mimi naomba nianze kwenye upande wa mapato.

Mheshimiwa Waziri amezungumzia mikakati tu mizuri kwamba mwaka huu wa fedha anategemea mapato yataongezeka, lakini alikojikita zaidi ni kwenye upande wa makusanyo ya kodi kwa maana anategemea kutoka kwenye Mamlaka ya Mapato. Lakini wakati anasoma Bajeti hapa leo tunazungumza kwenye fungu lake hasa, alitueleza wazi kwamba makusanyo ya mapato na mapato kutoka kwa wafadhili, lakini ataweka mkazo mkubwa kwenye vyanzo vingine ambavyo havitokani na kodi.

Sasa nilipokuwa naangalia hotuba yake, nikaona kwamba mwaka uliopita kwenye mapato ambayo yasiyotokana na kodi yalikuwa karibu na shilingi bilioni 313. Lakini mwaka huu ambao ameutilia mkazo zaidi inaonekana kwamba anategemea kukusanya shilingi bilioni 231.52. (*Makofi*)

Sasa nikawa najiuliza ile mikakati ambayo ameiweka hayo mapato yako wapi? Labda atatueleza kwamba unapoweka mkakati maana yake na mapato yanabidi yaongezeke. Sasa mara nyingi tumekuwa tukijikita tu kwamba kwenye kodi, jicho letu la mapato ya ndani ni kodi. Lakini kuna mapato ambayo hayatokani na kodi yamekuwa hayakusanywi. Sijui Mheshimiwa Waziri ameangalia upande gani, ameangalia vipi kwenye upande wa makusanyo wa magawio kwenye hisa mbalimbali, kwenye taasisi mbalimbali ambayo Serikali inamiliki. Kuna zile hisa ambazo ziko chini ya asilimia 20 mpaka 50 na mengineyo, analizungumzaje hili, je, hakuna mkakati ambao ameuweka ambao aliuzungumzia wakati anasoma Bajeti yake hapa ndani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini kuna mauzo ya Mashirika, vyombo mbalimbali, vifaa mbalimbali vya umma ambavyo hajavizungumzia sana. Mimi nilitaka nijikite hapo kwenye upande wa uuzaaji wa mashirika yaani kubinafsisha. Tumeachia *Consolidated Holding Corporation* kwa Mama Lupembe kwamba amekuwa akikusanya. Lakini mpaka sasa mashirika mengi tuliyobinafsisha waliweza kulipa asilimia 10, asilimia 25, ile *balance* mpaka leo hatujui imefikia wapi na kuna mkakati gani sasa. Kwa sababu wananchi wanafuatalia. Tumeona mfano kwenye sehemu mbalimbali,

wanafadhili, unapolipa *deposit* ya asilimia 10 au 25 wanataka wajue labda mmepe miaka miwili awe amemaliza kulipa, anaanza lakini hakuna kinachozungumzwa hapa kwamba amelipa au hajalipa na kama hajalipa hatua gani zinachukuliwa sasa kuhakikisha kwamba ile *balance* iliyobaki inalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inakuwa kama kiini macho kimojawapo. Tumejifunza sehemu mbalimbali, analipa asilimia 10, halafu baadaye Serikali hiyo hiyo inakuja tena kumwekea dhamana, anakopa ili aweze kuendeleza kile alichouziwa. Sasa nilikuwa nafikiria ni kuondoa mzigo kwa Serikali ili tuweze kuongeza mapato. Lakini kumbe mzigo ule unakwenda kubebwa na Serikali kwa njia nyingine tofauti, sasa hii imekuwa ikitupa wasiwasi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Kitengo cha Msajili wa Hazina. Tulikaan *Ubungo Plaza* pale walituwekea mikakati mizuri sana ya kuboresha. Lakini mimi bado nina wasi wasi, labda Mheshimiwa Waziri hapa atatuambia wakati anajibu, mkakati gani wa msingi ambao ameweka tangu tulipokaa *Ubungo Plaza* kukiimarisha Kitengo hiki cha Msajili wa Hazina? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, mimi naona bado kuna matatizo. Hapa umeweka mkakati kwenye hotuba kwamba tutahakikisha kwamba haya makampuni na taasisi mbalimbali za Serikali zinapeleka taarifa ya mahesabu yao kila robo mwaka inapofika. Lakini ukiangalia kile Kitengo kiko vile vile. Sina hakika na Mama Bukuku na mwenzake Mama Mlaki pale, kama wana uwezo wa kupitia haya mahesabu wakasema hapa tulitakiwa tupate gawio na hapa hatukutakiwa tupate gawio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho bado kimekuwa kikinitisha sana. Sasa Mheshimiwa Waziri, aseme hayo, ni mkakati gani ameuweka kwenye hiki chombo, kwa sababu unaweza ukasema tunapokutana na sisi tunakaa mwaka wa kwanza unapita, tutakapokutana tena mwaka kesho itakuwa ni hotuba ile ile, inazungumzia mambo yale yale. Sasa mkakati aliouweka ni upi. Upande mwingine, ni kwa upande wa Serikali kujitumbukiza kwenye kuweka dhamana ya kukopesha mashirika binafsi, watu binafsi, kwa *ku-guarantee* ikiamini kwamba yule mtu atalipa. (*Makofi*)

Sasa asipolipa je, Serikali imeshafanya tathmini Waziri atuambie katika dhamana zote mlizoweka kwa miaka hii yote ni kiasi gani mlishalipa na wapi ambapo mnadaiwa na mna mkakati gani wa kulipa kama yule mtu mliyemwekea dhamana hajalipa, ili itupe picha kamili kwamba hali ikoje, je, tutajikuta baadaye sasa tunarudi kule kule tulikotoka. Lakini ni vizuri mnapoweka dhamana ukawa unamdhaminu mtu ambaye una uhakika baada ya kuzalisha, baada ya kukaa kwa muda miaka ile ambayo mmekubaliana lile deni limelipwa na kama halilipwi Serikali waseme wana mkakati gani wa kutumia njia yoyote ya kuhakikisha kwamba lile deni linalipwa au la sivyo Serikali yenye we iweze kulipa kusudi wale wanaokopesha wasije wakaanguka kabisa wakapata matatizo na hili nalisemea wazi kwa sababu Kambi ya Upinzani nimeona hotuba yake hapa. Imebidi niliseme, wamesema kwamba mnadhamini mashirika na taasisi za Serikali na wengi wanaenda kwenye Mifuko hii ya Pensheni ingawa hii namba hapa iliyowekwa shilingi

bilioni 100 kutoka *NSSF* si sahihi itabidi wairekebishe, najua ni shilingi bilioni 12 ndizo *NSSF* walikopesha. (*Makofi*)

Sasa hii mifuko tutakayokuwa tunaibebesha madeni kwa kusema toeni, toeni halafu mwisho wake utakuwa nini? Mimi namwomba Mheshimiwa Mustapha Mkulo, kwa kweli atuweke wazi ili tujue Serikali ina mkakati gani kwenye madeni yote ambayo imeweka dhamana na yameshapita wakati na wale watu hawajalipa, watafanyaje ili waweze kulipa. Lakini tumekuwa na tatizo lingine la mfumuko wa bei, linanigusa hili kwamba Serikali mara nyingi imekuwa kimya kusema, halafu inaleta minong'ono, hatupewi sababu. Kuna wakati tulishakaa na Waziri wa Fedha wakati huo, tumekaa na Benki Kuu, tukaulizana kwa nini huwa hamtoi taarifa? Wananchi huku wananganung'unika bei za pembejeo zimepanda, mfuko wa *cement* umepanda bei, vifaa mbalimbali bei ziko juu. Ni lini, kwa nini wananchi wasiambiwe sababu, kwa sababu sasa kunakuwa ni kigezo cha kusema Awamu ya Tatu, vitu vilikuwa havipandi bei. Sasa tumeingia Awamu ya Nne, vitu vinapanda bei. Lakini kuna saabu za msingi ambazo wananchi wangeweza kuambiwa zingeweza kusaidia sana ili waweze kujua sababu si utawala uliopo au utawala uliopita, kuna sababu za msingi ambazo zinapelekea kwamba mfumuko wa bei uwepo. Lakini sasa kwenye vifaa kama vya ujenzi, kama *cement*, bati, mbolea na Serikali iangalie kwamba itaweza kuweka ruzuku kuwasaidia wananchi wakati bei zinapanda. Kuna malalamiko makubwa sana. Siku hizi wananchi wanaelewa sana, huwezi ukawaficha kitu. Kwa hiyo, tunapata maswali magumu sana ya kujibu. Inakuwa siyo rahisi sana kuwapa majibu ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumzie lingine ni kwa upande wa usimamizi wa Bajeti ya Serikali. Tumekuwa tukipitisha hapa Bajeti za matumizi na mapato. Lakini usimamizi wake umekuwa ni finyu sana, hasa kwenye pesa za maendeleo. Sasa pesa za maendeleo unaweka Bajeti baada ya muda unapokaa kuwahoji hawa watu waliopewa Bajeti, unaambiwa katikati ya mwaka kulitokea tatizo tukaambiwa turudishe tena shilingi bilioni 15, shilingi bilioni 15 au turudishe shilingi bilioni 20, shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kusaidia dharura iliyotokea. Lakini inapotokea hivyo hatuletewi taarifa huku ndani ya Bunge kwamba kuna dharura hii tumeamua kuitisha Bajeti hii, tumeamua kupunguza Bajeti kwenye mafungu mbalimbali. Lakini kuna vingine ambavyo vinatumika nje ya Bajeti. Sisi Bunge hatuna habari. (*Makofi*)

Sasa nilikuwa naomba ili kupunguza hoja nyingi za Mkaguzi wa Serikali, inapotokea suala hili hoja iletwe ndani ya Bunge kwanza. Mapendekezo yaletwe kama tulivyozoea huko nyuma, ili kama ni Bunge lipitishe. Kama ni *allocation of fund* ifanyike ndani ya Bunge kusudi kupunguza hoja za Mkaguzi. Upande mwagine wa mirathi na mafao ya wafanyakazi. Nimekuwa nikisikiliza sana maswali ya Waheshimiwa Wabunge hapa na mimi mwenyewe inanihusu, walimu wanataka kuandamana, lakini ukisema Mheshimiwa Waziri kwamba hiki kitu ni mtambuka inaanzia Wizara nyingi, Mahakama na haisadii sana, upange. Unaopewa lawamani Waziri wa Fedha. Kwa sababu watu wanajua kwamba pesa zinatoka wapi, Wizara ya Fedha. Sasa kwa upande wa mirathi, ingekuwa inawezekana Mheshimiwa Waziri ukasema wewe uvae wasikujue kama ni Mheshimiwa Mustapha Mkulo ukajua mlolongo wa kupata mirathi, ungekuja kutuambia ndani ya Bunge hili ni tatizo kubwa sana katika ufuutiliaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungefanya tu majaribio wala usijitambulishé kwamba mimi ni Mbunge au ni nani? Kuna tatizo kubwa. Mimi limenikuta na nafikiri na Wabunge wengi na leo asubuhi nimemsikia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wetu pale akilalamika na akisisitiza kwamba ule mkataba uko wapi? Unatekelezwaje? Alikuwa anaulizwa Waziri wa Katiba na Sheria hapa. Limekuwa ni tatizo, hivi ukisema siwalipi, kwa sababu watu wengine wamezidisha, mwalimu sikulipi, wengine wamezidisha pesa nyingi kuliko wanazodai. Hivi ni nani ataniambia mimi kwamba unachodai siyo sahihi? Unachodai hicho ulicholeta ni kikubwa kuliko kile unachostahili kupewa. Inatakiwa nijibiwe nipewe taarifa. (*Makofi*)

Mimi nimeleta malalamiko yangu, lakini najumlishwa kwenye kundi kubwa, tunaambiwa kwamba hamlipwi kwa sababu maombi yenu si sahihi. Hivi kweli siyo utaratibu kwa kweli Mheshimiwa Waziri. Mimi ningeomba nikushauri mlitchukuwa jukumu kwa niaba ya Serikali wakati ule malalamiko ya walimu awamu ya kwanza mkalipa, mkatuma wahasibu kwenye Wilaya zetu, wengine wakapewa na wengine hawakupewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wale waliobaki wenyé malipo ambayo hayastahili, wana haki ya kujibiwa na kupewa kiwango sahihi ambacho wanapaswa kulipwa, kuliko wakabaki wanalamika, mtu anasema anadai shilingi milioni 10 kumbe anadai shilingi milioni mbili.

Kwa hiyo, ni vizuri akaambiwa kwamba wewe unadai shilingi milioni 10, kujibiwa ni muhimu na ni haki ya kila Mtanzania kuliko wakabaki wanaendelea kulalamika. Kwa hiyo, ningependa sasa nisitisize kwamba ni vizuri tukawasiliana. Uwazi (*transparent*) ni muhimu ya Serikali ni muhimu ili watu wasiendelee kulalamika wakatumbukizwa kwenye kundi wale wanaostahili na wasiostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye madai ya Afrika Mashariki, nilimsikia Naibu Waziri hapa akisema kwamba njoo ni ofisini kwangu, mnione mimi. Si utawala bora. Lakini vile vile ukumbuke si rahisi mtu akaja akakuona akaingia ofisini kwako Waziri akuone. Sio rahisi, kwenye *system* ambayo ni sahihi kila mtu anajua niingie wapi, nitoke wapi na nipate majibu sahihi. Lakini mngejua majibu yanayojibiwa huko na baadhi ya watendaji yanakatisha tamaa. (*Makofi*)

Sasa atakapokuja hapo ofisini kuja kusema kwamba mimi ndiyo nadai, mimi ndiyo fulani, kwanza ule mlango wa kuingia mpaka akukute Mheshimiwa Waziri atakuwa amechukua siku nyingi sana. Kwa sababu kule Hazina Ndogo hayatoki majibu ya usahihi. Ukiwa *reception* hupati majibu ya usahihi mpaka aje akukute Mheshimiwa Mustapha Mkulo hapa ameshapiga *mark time* ya siku nyingi sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ningefikiri tuweke *system* ambayo itamwezesha kila mtu ajue wapi kwa kwenda na mwisho ningependa niseme kwa upande wa *PPF*. *PFF* kwa upande wa pensheni ya watu walioajiriwa na Mashirika ya Umma hapo zamani na mpaka sasa. Sheria ile tuliiptisha, tuliiirekebisha ile ya mwaka 78. Lakini bado kuna maswali mengi.

Vile viwango ni vidogo lakini pili zile pesa ambazo watu ambao hawajafikisha miaka 55 ya kustaafu watakuja kulipwa wakifikisha miaka 60 au 55. Ni tofauti kabisa na mifuko mingine kama *NSSF* wanaweka riba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *PPF* hakuna riba. Sasa hivi mtu aliyekuwa anapata wakati huo ana miaka 40 anapata shilingi 50,000/= sasa atapata ngapi akifikisha miaka 60. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Estherina Kilasi kwa kweli ulikuwa unaonyesha taaluma yako hapa kuisaidia Serikali yetu. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Job Ndugai, ajiandae halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze na mimi kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya na uzima ili na mimi kwa uzima nilionao niweze kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii na kuweza kuchangia mada ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii naomba na kwa ruksa yako kuwatakia kheri na fanaka Jumuiya zote za Chama cha Mapinduzi Mkoani Manyara kwa ajili ya kipindi hiki cha uchaguzi wakati ambapo wanatarajia kuchagua viongozi wa ngazi mbalimbali. Namwomba Mwenyezi Mungu awaongoze na kuwasaidia ili kukamilisha zoezi hili kwa amani na upendo na hatimaye kupata viongozi makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba sasa nitoe mchango wangu mfupi sana kuhusu Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza niungane na baadhi ya wachangiaji kuchangia kidogo tu kuhusu Ofisi ya *CAG*. Mimi kwa mawazo yangu nisingejali kuona kwamba Ofisi hii ya *CAG* ama Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inakuwa chini ya nani. Wengi wameshauri kwamba iwe huru na nadhani nia ya kutaka iwe huru ni kwa maana ya kwamba ili iweze kuwa na meno ama iweze kuchukua hatua kwa wale wabadhirifu ama wahalifu watakaobainika katika ukaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kwanza kabisa kazi ya udhibiti itakapokuwa *transparent* wabadhirifu watakavyoanikwa hadharani kabisa kwamba nani mhalifu, mbadhirifu, mwizi, nani kafanya vizuri, nani kafanya vibaya na wananchi wakajua bila kujali kwamba Ofisi hiyo iko chini ya Bunge ama chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi ama chini ya Serikali wahusika kwa vyovypote vile watachukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nadhani sheria ya kushughulikia wabadhirifu lisiwe changamoto. La muhimu ni kuchukua hatua ama kurekebisha sheria iliyopo. Kwa kuwa changamoto ni suala ambalo linakuwa nje ya uwezo. Lakini kurekebisha sheria ni suala ambalo Serikali inaweza ikalishughulikia haraka

iwezekanavyo na hasa tukijua kwamba suala hili limekuwa likipigiwa kelele kwa muda sasa. Kwa hivyo, sheria itakavyobadilishwa suala zima la kuinua uchumi linaweza kufanikiwa kwa haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kidogo kuhusu hili eneo la *public procurement* ama la manunuzi. Mimi ingawa sina ujuzi na eneo hilo. Nadhani wanaoshughulika na manunuzi kwa ajili ya mali ya Serikali wanapaswa kuwa wanasomea ama ni watu maalum katika taasisi za Serikali. Lakini ningetoa ushauri kwamba wanaoshughulika na manunuzi kwa sasa hivi aidha, hawajui sheria na ndiyo wana-take advantage ya kwamba Serikali haifuatili kwa umakini au kwa ukaribu suala zima la manunuzi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, eneo hili likiangaliwa vizuri na kwa umakini zaidi, nadhani suala zima la manunuzi ambayo hayakidhi ama yanapelekei ubadhirifu wa mali ya umma yanaweza yakarekebishika. Eneo lingine ambalo nataka kuchangia kwa ufupi ni kuhusiana na fedha zilizotoka kwenye akaunti ya *EPA* kwenda kwenye akaunti ya Serikali. Pengine hili ni mapema lakini kwa sababu Serikali imekwishatoa tamko, mimi naomba nilitolee tu maoni yangu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina maneno na mfuko huu kwenda kusaidia pembejeo ama kuongeza ruzuku kwa ajili ya pembejeo za kilimo. Lakini ninachoomba kwa sababu nchi hii ni ya wafugaji na wakulima, vile vile fedha hizi ziweze kuelekezwa kwenye akaunti itakayosaidia pembejeo kwa ajili ya wafugaji. Wafugaji wana matatizo makubwa japokuwa wakulima pia wana matatizo na kwa hiyo, kuendelea kuegemea upande mmoja ya wakulima peke yao na wafugaji wanazidi kuwa na matatizo, bado Serikali yetu haijaweza kuwasaidia wafugaji. Wafugaji bado wanabangaiza tu, ukieleza matatizo yao watakuambia kuna *Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* na sasa Serikali inaelekeza nguvu kuanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kuendeleza sekta ya uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nadhani tutaambiwa kwamba sasa na hili nalo lielekezwe upande wa uvuvi isaidie na mifugo. Nashauri kwamba ianzishwe programu maalum kwa ajili ya wafugaji kama *Livestock Sector Development Programme* jinsi ilivyo *ASDP*, ama vianzishwe vile vile benki ya wafugaji hilo halina tatizo kwa sababu kuanzishwa tu benki ya wakulima nadhani wafugaji bado watakuwa wameachwa pembeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali igawe matumizi ya mfuko huo ili nao wafugaji waweze kunufaika. Niongelee kidogo kuhusu benki ya wafugaji. Mimi nadhani wafugaji pia wana fedha nyingi sana kama vile wakulima walivyo. Kwa sababu wafugaji kwa uduni wa maisha yao nina hakika pia hawakopesheki na hata mifuko hii ya fedha, taasisi mbalimbali za fedha, *SACCOS* ama hata haya mabilioni ya JK nadhani wengi hawajawahi kusikia kuna kitu kama hicho. Kwa sababu hawanufaiki nacho. Watakapoanzishiwa benki yao, kutakuwa na utaratibu maalum ambaa utawenza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki ya wafugaji inaweza ikawahamasisha hata wakaacha kuhamahama. Wataweza kuhamasishwa kuuza mifugo yao wakati wa ukame wakaweka fedha benki na hatimaye wakati ukawa nzuri, wakaja kununua mifugo baadaye na kuendelea. Najua hili ni gumu sana kwa wafugaji. Lakini kuanzisha benki ni njia mojawapo ya kuwaendeleza wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ombi kwa kweli kuhusu benki hiyo muhimu ya wafugaji. Naomba nisisitize hilo na hasa nimeizungumzia hiyo kwa ajili ya mfumo ambaao utaelekezwa zaidi kwa wakulima kufuatana na fedha hizi za *EPA* itakapoanzishwa benki ya wakulima ianzishwe pia na benki ya wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi jioni hii sikuwa na mengi sana ya kuchangia. Ninaomba baada ya kusema haya machache, niseme naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Martha Umbulla kwa mchango wako na hasa kwa kuwajali wafugaji. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Clemence Lyamba, ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia jioni ya leo katika hoja iliyo mbele yetu na mimi nianze kwa niaba ya wananchi wa Kongwa naomba nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni wiki iliyopita ambapo alichambua mambo mengi sana yenye umuhimu wa kipekee katika nchi yetu na kupitia utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Nne kwa karibu nusu ya kipindi chake. (*Makofi*)

Kwa kuwa Mheshimiwa Spika amesema kwamba utapangwa muda maalum wa kujadili hotuba hiyo, nilikuwa na hamu sana ya kuipitia lakini basi nitakuwa na uvumilivu wa kusubiri wakati muafaka uliopangwa. (*Makofi*)

Lakini mambo mawili niyaseme kwa haraka haraka, moja namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulimaliza suala la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Tunaomba jambo hili lingeanza mapema iwezekanavyo ili mambo yawefe kwenda katika kuwasaidia wananchi katika miradi yao ya maendeleo.

Lakini la pili ninalomshukuru sana ambalo siwezi kuvumilia kusubiri ni suala la fedha la *EPA* kuamuliwa kwamba ziende zikasaidie wakulima kupitia Benki ya *TIB* na taratibu nyingine zitakazowekwa. Jambo hili nalipongeza sana. Ni fedha ambazo zitasaidia sana wakulima wetu katika masuala ya mbolea na mambo mengine. Lakini niseme tu hapa kwamba tunatarajia wafugaji nao watakuwa katika kundi hili linaloitwa wakulima. Wameachwa kwa muda mrefu sana. Ni vizuri na wao wakafaidika na fedha hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa fedha hizi zinapitia *TIB*, *TIB* ni benki kama benki nyingine, wakulima na wafugaji kwa kawaida ya masharti ya kawaida ya kibenki siyo rahisi sana wao kufaidika na fedha. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie kipekee namna ya kuwfanya wakulima na wafugaji wa Tanzania wakafaidika na mikopo

hii. Vinginevyo nayo itaenda kama mingine ilivyoenda. Mwisho wake madhumuni na makusudio ya Mheshimiwa Rais na ya Bunge hili yanaweza yasitekelezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimesimama leo, nadhani kesho, keshokutwa inaweza siyo rahisi kusimama kuzungumza kwenye *Financial Act* ambayo itafuata baada ya mjadala huu, ukurasa wa 771 ambayo itakuwa *moved* na Waziri wa Fedha, kuna kodi pale ambazo zimeainishwa. Kwa mfano, kabla ya kodi hizi ambazo zinapendekezwa tuzipitishe keshokutwa hapa kupitia hii *Financial Act* pato la chini ya shilingi milioni moja lilikuwa halikatwi kodi. Sasa hivi imeshuka imekuwa pato la shilingi 690,000/= badala ya shilingi milioni moja. Siyo tatizo sana, badiliko si kubwa hapo. Lakini kati ya shilingi milioni moja na milioni mbili kodi yake ilikuwa shilingi 35,000/= tu. Sasa hivi inapanda kutoka shilingi 35,000/= hadi shilingi 150,000=.

(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ongezeko sijui la asilimia ngapi? Ni kubwa sana, anayepata kati ya shilingi 2,000,000/= na shilingi 3,000,000/= alikuwa anakatwa shilingi 95,000/= katika mapendekezo mapya atakatwa shilingi 380,000=.

Sasa ninachokizungumza hapa ni nini, tunaweza tukawa tunaongeza mishahara ya wafanyakazi na mambo mengine lakini matokeo yake ni kwamba makato yanazidi kuwa makubwa unatoa kwa mkono wa kulia unachukua kwa mkono wa kushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemuomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili ili aliweke vizuri. Ongezeko lolote kwa wafanyakazi wetu na wananchi wetu katika kipato liwe na maana kwao kuliko kuwa na kodi hizi ambazo ni kubwa sana kwa wananchi na wakati mwingine wawekezaji wengine wakija hapa matajiri wakubwa wanakuwa na misamaha fulani fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni kumuomba Waziri Mheshimiwa Mustapha Mkulo na Manaibu wake na Wizara yake kwa ujumla, fanyeni mabadiliko ya msingi kabisa katika Wizara ya Fedha katika maeneo yafuatayo ili mkumbukwe baadaye kwa yale mliyoyafanya; eneo la malipo ya mishahara ya wafanyakazi na madai yao tunayoyasikia sikia haya na harufu za migomo ni za nini hizi? Kwa nini hamkai na wafanyakazi mkazungumza nao mkaweka mambo sawa sawa? Kwa nini tusiwalipe wafanyakazi wetu vizuri? Eneo hili lifanyieni kazi kuna hali kubwa ya kutokuridhika, si vizuri kujenga jenga hali za kutokuridhika hivi haipendezi, lifanyiwe kazi eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni malipo ya uezemi ya wastaifu wetu. Wenzangu wamezungumza hata kabla yangu. Lakini vilevile malipo ya mirathi kwa wajane na wafiwa, wanateseka sana Watanzania hawa. Sisi Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi kwenye majimbo yetu tunapata malalamiko ya aina kwa aina kuhusiana na masuala ya mirathi na malipo ya uezemi kwa wastaifu mbalimbali. Malalmiko gani?

Kwanza baadhi ya malipo ni madogo sana hasa waliostaifu miaka ya nyuma kidogo. Wengine malipo yao ya mwezi hayatoshi kumuwezesha mstaifu huyu akasafiri hadi kule mkoani anakoenda kupata fedha zile, haitoshi hata kwa nauli ni malipo ya ajabu. Hivi ni kwa nini tusiweke *minimum standard*? Kiwango ambacho kwa mfano

unasema atakayelipwa chini kabisa atapata nusu ya kima cha chini cha wakati huo? Kwa nini tuwalipe watu wetu vichekesho? Ni watu waliofanya kazi kwa bidii sana katika nchi yetu, kwa uaminifu mkubwa, wamefanya kazi mpaka wamestaafu, leo tunawalipa vitu vya ajabu kwa nini? Kuna sababu gani ya msingi katika jambo hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *group* hilo wako Makatibu Wakuu wa zamani na Makatibu Wakuu wa sasa mpo, mnaona wenzeni wanalipwa vichekesho, mnaona sawa tu maana yake haiwagusi. Wako walimu, wako waganga, wako manesi, wako askari, wako watu wa kila kada, watu waaminifu kabisa kabisa, walijitolea katika nchi yetu kufanya kazi ambayo ndiyo imetuwezesha sisi leo tuko hapa lakini wanalipwa vichekesho, hivi hata hii nayo inahitaji kweli Bunge liunde Tume ya kuangalia ni kwa nini Watanzania hawa wanahangaika hawapati malipo vizuri, hatulioni hili? Wanaishi kwa taabu sana hawa, ni kwa nini tunaibeba dhambi hii? Tunatoa ujumbe gani kwa vijana wa leo ambao wanafanya kazi? Tunadhani kwamba wale hawaoni au hawaelewi? Mlolongo mkubwa na taratibu nyingi zinazokinzana katika kuwalipa wastaaafu wetu na wafiwa, wengi wamekata tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanikumbusha enzi hizo nilipokuwa shule tulikuwa na wanafunzi wa kutoka nchi mbalimbali kama Zambia, Zimbabwe, Namibia, Botswana, Malawi, Kenya na Uganda, hizi za hapa karibu Mheshimiwa Mgana Msindai anafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yetu wanafunzi wa Kitanzania yalikuwa tofauti sana na wanafunzi wa nchi hizi tofauti kabisa. Mkikaa ninyi Watanzania mnawaza habari ya Mungu akipenda, ikiwezekana, miaka minne mitano niwe nimejenga kajumba kangu, ndiyo mawazo ya Mtanzania. Mawazo hayo hawa wenzetu hawana kabisa, nikawa nashangaa hawa mbona wanawaza tofauti maana wao watakapoenda kazini wana uhakika wa nyumba kubwa yenye samani, akitaka gari anaenda kukopa, mambo yake ni sawasawa hawazi ujisadi, ujisadi. Sisi vijana wetu toka wadogo, wameshaelewa kabisa kwamba nisipochangamka mwenyewe kwa nafasi yangu mimi nimekwisha kwa sababu ya utaratibu huu wa kuwaona wale waliofanya kazi kwa uaminifu mkubwa wanahangaika mtaani, hawana *future*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu ni mtu mwenye akili sana hawezi kukubali ninyi tu Serikali mumtumie yeye kama dodoki halafu akizeeka mumtupe hapo, haiwezekani. Na mnawaona vijana wetu kweli, ukimuajiri sijui kama kuna wanaopitisha miaka mitatu, minne hawajajenga. Na wamejenga kweli kwa uwezo wao ndani ya kipato halali? Sasa huu ni msingi ambao tumeujenga, lazima kabisa tuuangalie, msingi huu si sahihi hata kidogo. Lazima turekebishe mambo haya watu walipwe vizuri, vijana wawe na matumaini. Tusiwajengee taratibu za kuwapa majaribu na matamanio, hasa huko Wizara ya Fedha. Unamlipa mtu kichekesho *ana-handle* mabilioni ya fedha, hapana tuliangalie jambo hili, watu walipwe vizuri. Hata Wabunge wastaaafu, Waheshimiwa ninyi mnafahamu, wanaishije huko nje? Hata sisi kesho, keshokutwa, baadhi yetu au baadhi yao ambao hawatarudi mwaka 2010 hatma yao ikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niko Arusha pale, tulikuwa na Wabunge wa Kenya, alikuwepo Mbunge mmoja mstaafu wa Kenya na Mbunge ambaye yuko kwenye Bunge la Kenya hivi sasa. Yule Mbunge mstaafu akawa anamwambia Mbunge aliyeo sasa, “Ninyi mnajilipa sana bwana, mnajilipa hela nyingi hamtukumbuki sisi wastaafu ambaeo na sisi tulikuwa Bungeni. Tunahangaika.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule Mbunge wa sasa akasema, ni ujinga wenu, ninyi mlikuwepo kwenye hilo Bunge wakati huo kwa nini hamkurekebisha mambo yenu? Mkakaa tu pale mnapiga piga makofi mnategemea sisi leo ndio tuwazungumzie ninyi? Jamani kazi kwenu, mkitegemea watu wengine waje wawasemee haya, tusilaumiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninalotaka kulizungumza ni suala la kuhamia Dodoma. Wiki iliyopita kuna Mheshimiwa mwenzangu mmoja alizungumza akakumbushia kwamba kuna mjadala unataka kuja kuhusu ama kuhamia ama vipi? Ningependa kukumbusha tu kwamba jambo hili la kuhamia Dodoma kwa sisi Wabunge wa *CCM* liko katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010, ni katika orodha ya mambo ya kuyatekeleza. Kwa nini katika ilani nzima lichomolewe la kuhamia Dodoma ndio liwe mjadala?

Kuna sababu gani za msingi? Hili linatoka wapi hili? Bunge tumehamia Dodoma, kwani asiyetaka kuhamia Dodoma ni nani hasa? Na uamuvi huu ultolewa wakati gani? Siku nyingi. Tena ultolewa na *founding fathers* kwa sababu nyingi tu, na sababu nyingi kati ya zile bado zipo. Kama sisi tulipo leo hatuna mpango wa kuhamia Dodoma kwa nini tunataka tubadilishe huo utaratibu? Kwani mmelazimishwa mhamie leo Dodoma? Ninyi kaeni Dar es Salaam, watahamia wenzeni watakaoku baadaye. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa kuhusiana na mjadala wa Mwenyekiti, wetu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kanuni namba ngapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni namba 64(1)(a).

**MWENYEKITI:** Taratibu taratibu, Kanuni namba 60 na?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64; “Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayoilinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge,

Mbunge, (a) Hatatoa ndani ya Bunge, taarifa ambazo hazina ukweli. (b) Hatazungumza jambo ambalo haliko kwenye mjadala.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wa Kitaifa unaotarajiwa hapa Dodoma na Dar es Salaam katikati ya mwezi Oktoba hauhusu kuhama au kutokuhama Dodoma, kwa sababu uamuvi wa kuhamia Dodoma ni uamuvi uliokwishafanywa na hakuna mtu ambaye anaweza akaugeuza. Mjadala ni utaratibu bora zaidi wa namna ya kuhamia Dodoma katika mazingira mapya ya karne ya 21. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo hapa unachotaka kusema ni kwamba hakutakuwa na mjadala unaohusu suala hili la kuhamia Dodoma ama hakutakuwa na kitu gani? (*Makofit*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima nataka kurejea kwamba mjadala hautahusu kuhamia au kutokuhama. Kwa sababu kuhamia tumekwishaamua, mjadala utahusu namna bora zaidi ya kuhamia Dodoma. Utaratibu bora zaidi kuliko ule wa mwaka 1973, utaratibu bora zaidi wa karne ya 21. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Lakini Waheshimiwa Wabunge, kama nimemsikia mchangiaji, yeze anachosisitiza ni kwamba katika mjadala unakubali Mheshimiwa Waziri utakuwepo, lakini anachosisitiza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mjadala uendelee *ku-focus* suala la kutekeleza ilani ya uchaguzi kuhamia Dodoma. Kwa hiyo, sioni kama mchangiaji ametoka nje ya hilo kwa mandhari kwamba Waheshimiwa Wabunge labda mnegeniskiliza nimalize *rulling* yangu kabisa, kwa maana ya kwamba mjadala uko pale pale na umekubali utakuwepo lakini kitu cha msingi, usihamishe lengo mahsusla la kuhamia Dodoma na ndilo wazo la mchangiaji. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba mchangiaji anaweza kuendelea, alikuwa katika hoja hiyo hiyo ya kuhamia Dodoma. (*Makofit*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na msisitizo wangu uko hapo. Kwa kweli nikisema mawazo yangu nashangaa hata mjadala ni wa nini? Tunatakiwa tuhamie Dodoma. Serikali inatakiwa ije na programu hapa ya kuhamia Dodoma, sasa hii maneno ya mjadala isije ikawa ni ujanja ujanja hivi wa kutaka, hayo ndio mawazo yangu nasema mapema kabisa. Ni uamuvi wa maana kabisa huu, kwa nini hatuitekelezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge limehamia Dodoma, leo mwaka wa ngapi? Lakini hata Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, haiko Dodoma iko Dar es Salaam, yeze mwenyewe hajahamia Dodoma. Hiyo inanipa wasiwasi kuhusu kuhamia Dodoma, inanipa wasi wasi kuhusu nia ya kuhamia Dodoma na hapa hapa nitoe wito, kwamba ofisi ya kwanza ambayo mimi napendekeza ihamie Dodoma ni Ofisi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Bunge, ambapo Bunge lipo, halafu nyingine zitafuata. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Ofisi hiyo kuhamia Dodoma napendekeza taasisi za kielimu Dodoma iwe *city of excellence*. Taasisi nyingi zaidi za kielimu

zijengwe hapa, napendekeza hospitali ya Apollo, India ambayo ina nia ya kujenga hospitali itakayohudumia Afrika Mashariki kwa magonjwa mengi ya wananchi wetu wanaoenda India, ijengwe Dodoma. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Rufaa, wanazo fedha hivi sasa za kujenga jengo, nashangaa wanapanga kujenga jengo lao Dar es Salaam! Kuna sababu gani Mahakama ya Rufaa isijenge jengo Dodoma na fedha wanazo hivi sasa? Na Serikali wanaona kabisa hawa wana fedha wanajenga Dar es Salaam, kwa nini hawajengi Dodoma? Wale Majaji 15 wa Mahakama ya Rufaa hakuna nafasi ya kuwa-*house* hapa na watumishi wao? Mbona hili linawezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kisingizio kilikuwa maji, leo mji wa Dodoma ndio mji wenye maji mengi kuliko mji wowote Tanzania. Kisingizio kilikuwa watoto wetu wasoma wapi? Leo tunajenga Chuo Kikuu kikubwa kuliko vyote hapa. Nilichosimama kukizungumzia kwa nia njema kabisa ni ile nia ambayo ilipitishwa na viongozi wetu waanzilishi ya kuhamia Dodoma, naomba mtu asiiguse. Kama sisi tuliko leo akina Ndugai, hatuwezi kuhamia Dodoma tuwaachie watakaokuja kesho wataangalia uwezekano kama wataweza watahamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Job Ndugai, na naomba sasa nimuite Mheshimiwa Clemence Lyamba na atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle Shibuda, sidhani kama ameingia? Kama bado hajaingia basi atafuatiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi. (*Makofi*)

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mada iliyo mbele yetu jioni hii. Nianze kwanza kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, akisaidiwa na Naibu Mawaziri wawili, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ambao wamehusika katika kuandaa hotuba hii aliyoitoa Mheshimiwa Waziri. Hotuba hii imeandalika vizuri, inaeleweka na imejieleza kwa umakini mkubwa, natoa pongezi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kujizuia kutoa pongezi mahsus na za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hivi karibuni, majuzi. Amekata ngebe ya wengi ambao walikuwa na nyodo juu ya Serikali yetu na kwa hakika hotuba yake imerudisha imani kubwa kwa Watanzania kwa ujumla na hii inatupa nguvu hata sisi Wabunge kusonga mbele na vifua mbele kwa bidii zote. Naona pia ni muafaka nitoe pongezi maalumu kwa Mheshimiwa Spika, kwa jinsi alivyo *sum-up* kwa zile dakika tano za mwisho, kwa sababu aliwakilisha mawazo ambayo ninaamini yalikuwa yamo katika roho zetu katika akili zetu sisi Wabunge wote. Baada ya pongezi hizo naomba sasa niende kwenye kuchangia mada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili tu mafupi sana kwa sababu nilikwishayazungumza katika hotuba ile kubwa ya Bajeti ya Serikali. Jambo la kwanza ni

suala la tozo ya VAT ambayo mimi na jirani yangu Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Castor Ligalama, tulilieleza kwa kirefu wakati tukichangia katika Bajeti kuu ya Serikali kwamba kwa muda mrefu tangu mwaka 2004 wakulima wa miwa wamekuwa wakitozwa tozo la VAT kwa huduma za gharama za kukata, kupakia miwa na kusafirisha miwa inayopelekwa viwandani kwa ajili ya kutoa sukari. Sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu alipokea suala hilo na akaahidi kwamba kwa sababu ni suala ambalo limedumu kwa miaka mingi tangu mwaka 2004 na kilio chetu ni dhahiri kwa sababu wakulima wadogo wadogo wale wana umoja wao ni kama ushirika na huduma hizo zinazozungumzwa na kukatwa VAT zinatokana na huduma zinazosimamiwa na kuendeshwa na Chama chao cha Wakulima kwa hiyo, kwa kweli hawakustahili kukatwa VAT au kuwekewa tozo ya VAT. Kwa kuzingatia uzito huo Mheshimiwa Waziri, aliahidi kwamba angelifanyia utafiti suala hili haraka sana ili hatimaye atakapokuwa akiwasilisha hotuba yake ya majumuisho ya hoja za Wabunge, atalitolea majibu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimesimama hapa kukumbushia na kumuomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa akitoa majumuisho nitamshukuru sana endapo atatoa kauli ili kuondoa kero hii ambayo imedumu kwa muda mrefu sana na ni kero kubwa kwa wakulima wadogo wa miwa ambao wanazalisha karibu miwa inayotoa 50% ya sukari inayozalishwa hapa nchini, hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nigosie kidogo sana, limeshazungumzwa lakini nashindwa pia kujizuia ni suala la malipo ya pensheni kwa wastaifu. Msemaji aliyezungumza hivi karibuni amedokeza juu ya kiwango kidogo cha malipo ambayo hata nauli hayakidhi kulipa kuwezesha kumfikisha mstaafuli katika ofisi ya mkoa kwenda na kurudi. Kwa malipo ya shilingi 21,000/= kwa mfano wengi wanarudi bila kitu. Malipo hayo ni kidogo sana, wastaifu wanaadhirika na sisi wote humu ndani, hapana sio wote, baadhi yetu ni wastaifu watarajiwa lakini wengi zaidi ni wastaifu watarajiwa.

Kwa hiyo, yale tutakayoamua leo si kwamba tu yatawanusuru ambao tayari wamestaifu lakini yatawasaidia na wale waliomo humu ndani ambao wanatarajia kustaifu katika miaka michache ijayo. Kwa hiyo, ni budi kwa kweli tukayatizama mambo haya kwa jicho la huruma na kufikia tamati ya maamuzi ya kuongeza hizi pensheni mapema iwezekanavyo. Kauli ya Serikali ilikwishatoka kwamba wanatarajia mchakato wa kuongeza viwango vya pensheni ambao utakuwa umekamilika mwezi wa tano mwaka 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mbali mno, kulikwisha kuwa na kauli huko nyuma iliyosema mchakato huu ungekamilika mwezi wa kumi. Mimi naomba kwa *spirit* aliyoieleza Mheshimiwa Spika, wakati aki-*summarize* hotuba ya Mheshimiwa Rais, alidokeza juu ya *speed* ya utendaji na utoaji wa maamuzi kwa watendaji Serikalini. Mimi nafikiri wakijipanga vizuri Serikalini inawezekana kabisa Muswada huu ukawenza kuwasilishwa katika Bunge hili katika kikao cha 13 mwezi Novemba. Naomba Mheshimiwa Waziri na timu yake mahiri wajitahidi kuuleta Muswada huu katika kikao cha 13 ili tuwanusuru wastaifu na adha ya muda mrefu ambayo imekuwa ikiwakumba na wao wakiendelea kuonyesha ustahimilivu wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limejitokeza kwenye masuala ya wastaafu hivi karibuni ni suala la kupanda kwa nauli za usafiri. Ni kweli ni wao wenyewe katika miezi michache iliyopita walikuwa wametaka kulipwa kila mwezi, lakini tayari wao wenyewe baada ya nauli kupanda kwa kiwango kikubwa sasa imekuwa ni kero kubwa wanashindwa hata kwenda na kurudi kwa malipo haya ya shilingi 21,000/= au karibu na kiwango hicho.

Kwa hiyo, basi mimi nilikuwa nina wazo kwamba ingekuwa ni vizuri Serikali ikachukua *initiative* ili kuwasaidia kuwanusuru katika adha hii iwasiliane na wawakilishi wa wastaafu, nafikiri wana umoja wao, ili waangalie uwezekano wa kuwalipa kila baada ya miezi mitatu ili waweze kusafiri kwenda na kurudi kuliko ilivyo sasa kwa jinsi walivyotaka awali malipo ya kila mwezi. Hii itawasaidia angalau mtu ukiwa na shilingi 60,000/= kwa malipo ya mkupuo yatakusaidia angalau kwenda na kurudi na ukabaki na fedha kidogo mfukoni. Kwa hiyo, yangu kwa kweli niliyokuwa nina nia ya kuyaweka mezani jioni hii ni haya lakini yote kwa yote naunga mkono hoja, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji na labda kabla hatujaendelea nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ibrahim Sanya, wote kama mlivyoona mgeni wetu wa leo amefanana sana sana na Mheshimiwa Ibrahim Sanya. Kwa hiyo, kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Ibrahim Sanya na tunamtakia kila la kheri huko mbele labda mambo yake yanaweza kuwa mazuri kama mtu aliyanayi nae alivyo katika hali aliyonayo kwa sasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya kumpongeza Mheshimiwa Sanya, naomba nimuite Mheshimiwa Esther Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi jioni hii niweze kuchangia Wizara yetu hii ya fedha na uchumi. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kabisa Rais kwa kuliona hili na kuunganisha Wizara zile mbili na kuwa Wizara moja ya Mipango pamoja na Fedha ili sasa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii tukunyoshee mkono vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kushukuru kabisa kuona sasa Mheshimiwa Mustapha Mkulo, uchumi anao, fedha zote za nchi hii anazo yeye, sasa kazi kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina wanamipango ambao wanapanga mipango yote ya nchi hii na Wizara hii imesimamia ukusanyaji wa fedha zote za nchi hii na kusambaza katika Wizara zake na huko vijijini kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yanaenda vizuri. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, uchumi wetu ukishuka sisi na wewe na maendeleo yetu yasipoendelea sisi na wewe. Munguakupe nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Rais pamoja na Waziri na kumtakia kila la kheri katika Wizara yake hii ngumu na ni nzuri kabisa ya utekelezaji tu, basi naomba niingie katika nafasi nyingine ya kuzungumzia Chuo chetu cha Mipango cha hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tuna chuo kimoja tu na bahati nzuri mimi kila mwaka huwa nasimama kwa kweli kukisemea hiki chuo na sasa hivi kwa kweli ndio kinaonekana chuo halisi cha wanamipango. Nikuombe sasa Waziri, chuo hiki umepewa wewe na hawa ndio wataandaliwa ili waweze kuweka mipango ya nchi hii katika hali ya kulipeleka Taifa letu katika maendeleo zaidi. Chuo hiki huku mwanzoni kilikuwa na masomo machache lakini sasa katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, chuo hiki sasa kinatoa Cheti, Stashahada, Shahada na kinatoa Stashahada ya Uzamili. Chuo hiki zamani kilikuwa pale eneo la Kiwanja cha Ndege, eneo lilikuwa finyu sana, tukashukuru Wizara ya Mipango wakaona chuo hiki kipewe eneo kubwa sana. Sasa hivi ukienda katika chuo hiki kwa kweli tumepiga hatua kubwa sana na naomba niipongeze sana Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda pale kwenye Chuo cha Mipango, kama nilivyoleza masomo ambayo yanachukuliwa pale wanaendelea na ujenzi amba ni wa kukamilisha ujenzi wa ukumbi pamoja na jengo la kwanza la taaluma. Ni kwamba Mheshimiwa Waziri kwa sababu sasa na fedha wewe ndio unazitoa nikuombe sana ili tuharakishe kuinua yale majengo yaweze kutumia fedha basi zote ziende kwa wakati. Tusiwe tena tunasuasua kutoa kidogo kidogo, pamoja na kwamba tunatumia *cash budget* lakini ulione hilo katika kukiendeleza chuo chako cha mipango ili kiweze kuendelea vizuri. Lakini cha kusikitisha sana nimeingia hapa Bungeni mwaka 2000 na bahati nzuri sana nikawa nimepangwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, Wizara mbili hizi zilikuwa pale. Kinachonisikitisha sana ni Serikali mna kigugumizi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kama hiki ambacho kinaendesha taaluma kama hizi kinatengeneza wanamipango kiasi hiki nilichozungumza hapa nyuma ni kwa nini sasa Serikali inakuwa na kigugumizi? Tangu mwaka 2000 Mkuu wa Chuo ana kaimu, ana kaimu, ana kaimu? Na mnakaimisha mpaka lini? Hii inasikitisha sana mtu mnakatisha tamaa, anakiendeleza chuo hicho, mipango yake ni mizuri tu, chuo kinaenda vizuri, wala hamna migomo kama vyuo vingine, lakini bado hatumpi haki yake ya kuhakikisha kwamba na yeye basi mnampa motisha kuona kwamba na yeye anakisimamia hicho chuo. Sasa mimi nasema leo mara ya mwisho, mwaka kesho naomba ukaimu uishe, mtu mpeni haki yake. Mimi simtaji, wewe unamfahamu kwa sababu yuko chini yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii nashangaa sasa Mkaguzi Mkuu, tena bado yuko kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi! Naungana na wenzangu kabisa kumuombea Mkaguzi Mkuu wa Serikali ajitenge, ajitegemee mwenyewe ili awe na haki ya kutenda wakati anapokagua mahesabu ya Wizara hii. Unapomuweka katika Wizara ya Fedha na Uchumi unampa *vote* yake aombewe na Waziri unamnyima haki yake, nikuombe Waziri basi muandae angalau utaratibu wa kuhakikisha basi mwenzetu huyu Mkaguzi Mkuu wa Serikali tukimpa haki ya kuhakikisha kwamba fedha za wananchi zinatumika vizuri, mtenge katika Bajeti yako angalau na yeye ajitegemee. Hili linalewaka nafikiri

Mheshimiwa Waziri atakuwa amelisikia na Wabunge wengi wamelizungumza. Kwa hiyo, mimi naomba niishie hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa kuwashukuru sana na kuwapongeza sana *TRA*, Mamlaka hii ya *TRA* ni peke yake ambayo imetufikisha mahali hapo. (*Makofi*)

Sasa hivi katika ukurasa wa 11 katika hotuba ya Waziri wanasema lengo lilikuwa ni shilingi trilioni 3.18 lakini kwa kazi nzuri waliyoifanya fedha halisi walizopata ni shilingi trilioni 3.35, ni pongozi kubwa sana kwa Mamlaka hii ya kusimamia ukusanyaji wa mapato. Naomba wenzetu tuwape moyo ndugu zetu wa *TRA*. (*Makofi*)

Lakini nimuombe Mheshimiwa Waziri bado huwa natoa tahadhari, kazi ya ukusanyaji wa mapato ni ngumu sana, je, tumewawekea mazingira gani hao wafanyakazi wa *TRA*? Tumewawekea Bima? Tunawapa motisha ya kuhakikisha kwamba wasiwe na tamaa ya kwamba fedha wanazokusanya kwa wakwepa kodi zote zinaletwa Serikalini? Naomba muwaangalie watu kama hawa ambao wanatupa nguvu kwa kuhakikisha kwamba kweli kazi wanafanya na kweli kazi inaonekana. Hili Waziri alizingatie na aone kwamba wafanyakazi hawa wanafanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi karibuni *TRA* Dar es Salaam wametoa utaratibu kwamba ukusanyaji wa kodi za majengo wataanza na Mkoa wa Dar es Salaam. Nikuombe Mheshimiwa Waziri uwe na maandalizi mazuri ya kuhakikisha kwamba wananchi ambao wanaguswa na hili zoezi la ulipaji wa kodi kwa sababu walikuwa wamezoea kulipa katika Halmashauri zao kwenye Manispaa. Je, utaratibu umeshauandaa vizuri? Isije ikafika mahali watu wakawa hawajui wanakwenda wapi na tukapunguza mapato, niombe elimu ya kutosha kuweza kuwaelimisha na mafanikio basi mje mtueleze ili kama tunasonga mbele ili tusije tukarudi nyuma tena na kuona kwamba mapato yetu yanashuka. Nina tegemeo kubwa sana kwamba elimu ya kutosha itatolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ulipaji wa pensheni. Mheshimiwa Waziri akubaliane na sisi kwamba suala la ulipaji wa pensheni bado manung'uniko ni mengi na yapo kwa wananchi waliopo huko vijijini. Kinachosikitisha sana ni kwamba kwa mfano watu wanakuwa wamekamilisha kwa mfano wajane, wanakuwa vile vikao vyta familia wamekamilisha kila kitu na Mahakamani lakini inapofika mahali wakati wa kulipa sasa anakuwa anazungushwa na ukiona kwamba ni malipo haya yanafanywa mikoani kwenye Hazina Ndogo za Mikoa na wananchi hawa wanatoka Wilayani kule. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba watu wanalipwa vizuri lakini aliangalie hili basi ili huduma hii ya Hazina Ndogo katika Mikoa hakuna uwezekano wa kufikisha hata kwenye Wilaya ili kupunguza gharama za hawa wastaifu ambao wanatoka vijijini wakapunguza gharama za kwenda mijini. Mheshimiwa Waziri nakuomba uje na mkakati wa kuwawezesha hawa wastaifu ili wawe wanasegezwa huduma zao katika maeneo ambayo wapo karibu nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni misamaha. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake amesema kwamba wataangalia misamaha ambayo haiwanufaishi Watanzania. Nakubaliana naye kabisa na sheria ikiletwa kwa kweli sisi

tupo tayari ila katika kuangalia misamaha hasa misamaha ya madini mimi nina wasiwasi nayo kabisa, imezidi imetupunguzia sana fedha zetu. (*Makofi*)

Lakini kabla ya kwenda kwenye misamaha mingine naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutueleza kwamba kufikia tarehe 20 wafanyakazi wote mishahara huwa wameshalipwa, kwa hilo nawapa pongezi sana Wizara hii na ninaomba muendeleee vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nazungumzia suala la msamaha wa kodi kwa wazee. Tarehe 05 Oktoba, 2005 Rais wetu Mstaafu wa Awamu ya Tatu alitoa agizo kwamba wazee ambao wanaishi katika nyumba zao hawana uwezo wa kulipia kodi za majengo yao wasamehewe, na bahati nzuri Waziri wa TAMISEMI wakati huo mwaka 2005 ambaye sasa hivi ni Waziri Mkuu alipeleka Waraka kwa Wakurugenzi maeneo hayo lakini cha kushangaza wazee hawa wanahangaika, naomba Waziri hili aliangalie wazee hawa washughulikiwe kama ilivyoagizwa na Rais na agizo likitolewa na Rais wengine ni watekelezaji. Wakurugenzi wa Halmashauri wanasema kwamba sisi hatujapata waraka, lakini agizo limeshatoka la Rais wa Awamu ya Tat. (*Makofi*)

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la wazee, nchi isiyokuwa na wazee kwa kweli si nchi, hebu tuwajali wazee maana yake wazee hawa wamekuwa wakihangaika katika afya, Waziri akiagiza kwamba watibiwe hawatibiwi, sasa hata kwenye kodi zao za nyumba itakapofikia basi tuwaone na hawa wazee na wenyewe tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, *TRA* izungumze nao wazee na wahakiki kweli kama ni nyumba zao na Rais aliagiza kwamba zisiwe nyumba za biashara, mimi siwatetei kabisa ambao wana nyumba za biashara, nyumba wanazokaa wenyewe wanazoishi, nafikiri ndiyo hizo ambazo Rais alikuwa amezimaanisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi sina maongezi mengi sana ya kuzungumza, ila nilikuwa nazungumzia benki ambayo Rais wetu juzi katika hotuba yake amesema fedha zile za *EPA* zitawekwa kwenye Benki ya *TIB* ya kukopesha wakulima, wafugaji na wavuvi. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aisimamie sana hii benki ili inapowakopesha hawa wakulima, wafugaji na wavuvi ile riba wasifanye kutoa mikopo yao kulingana na biashara ambayo kama benki nyingine zinavyofanya. Naomba sana waangalie riba ambayo watamudu wakulima, wafugaji na wavuvi ili waweze kumudu mikopo watakayochukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nilikuwa na machache tu ya kuzungumza ya kukupongeza kwa kazi nzuri ambayo Waziri anaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu ule ule tu wa kiti, orodha niliyonayo hapa yote ni ya Wabunge wa Chama Tawala na ndiyo maana sasa kwa kuweza ku-*balance* michango Bungeni nitamuita Mheshimiwa Kabwe Zitto halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Fedha na Uchumi, Wizara ambayo kwa jinsi ambavyo imeunganishwa inashughulikia sehemu kubwa sana ya uchumi wa nchi yetu, inasimamia mambo mengi sana, inasimamia sera mbalimbali za kiuchumi na za kifedha, ina vyombo mbalimbali muhimu na nyeti katika maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, ninafarijika sana kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kabla sijaendelea katika maeneo ambayo nataka kuchangia niwatahadharishe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kazi ambayo tumeifanya takriban kwa mwaka mmoja uliopita, ambapo Kambi ya Upinzani Bungeni imefanya kazi kwa juhudhi kuonyesha jinsi gani ambavyo Taifa liliibiwa mabilioni ya fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania na bahati mbaya sana wenzetu wa upande wa pili walikuwa wanatuona kama tunasema uongo, leo ndiyo wamekuwa pamoa nasi kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika. Lakini sisi tunafarijika sana kwamba tumetekeleza wajibu wetu wa Kikatiba kama Kambi ya Upinzani, naamini kabisa kwamba uchaguzi ujao utakapokuja wananchi wataona kwamba sisi ndiyo tutakaokuwa na uwezo wa kuweza kulinda rasilimali zao. (*Makofii*)

Lakini pia naiambia Serikali kwamba ijaribu kuangalia taratibu za Kikatibu na za kisheria zinavyopaswa kufuatwa kutoptana na mali za umma. Kwa mujibu wa sheria zetu, fedha ambazo hazina mwenyewe au mali yoyote ambayo Serikali inaiona haina mwenyewe ni mali ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, Serikali ni lazima ifuate taratibu za kisheria kuhakikisha kwamba mali ile inaingia katika mali za Serikali na wenye jukumu la kugawa fedha au mali hizo ziende wapi ni jukumu la Bunge, siyo jukumu la tawi la utendaji na siyo jukumu la *executive*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nilikuwa napenda niikumbushe hivyo Serikali maana yake ni rahisi sana watu kuanza kuandamana na kadhalika kushereheke, lakini jukumu la ugawaji wa fedha ni jukumu la Bunge siyo jukumu la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siyo jukumu la Waziri Mkuu na siyo jukumu la Waziri wa Fedha bali Waziri wa Fedha anapaswa kuja kuomba kibali hapa kwa taratibu ambazo tumeziweka. Kwa hiyo, napenda suala hilo niweze kuliweka ili liweze kueleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima la Ofisi ya Msajili. Mama Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Hesabu ya Mashirika ya Umma amelizungumza vizuri sana. Mimi nataka nikazie zaidi ya kwamba kwa mujibu wa sheria, Ofisi ya Msajili wa Hazina ni *Corperation Sole* kwa hiyo, inapaswa kufanya kazi katika hali ambayo ni ya uhuru zaidi sivyo ambavyo inafanya kazi sasa hivi kama idara fulani ndani ya Wizara ya Fedha na bahati nzuri sana Waziri wa Fedha wa sasa amewahi kuwa Msajili wa Hazina, kwa hiyo, matatizo ambayo tunayazungumza

anayafahamu na tungependa kwa kweli ndani ya mwaka huu wa fedha suala hili la jinsi gani ambavyo Ofisi ya Msajili wa Hazina inafanya kazi liweze kushughulikiwa inavyopaswa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivi sasa tuna jumla ya mali zenyе thamani ya dola bilioni 4.4 yaani zaidi ya trillioni 5 ambazo zinasimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ukiangalia ile *statement of interest* na *investment* ya Serikali kwenye Mashirika mbalimbali inasimamiwa na Ofisa Msajili wa Hazina. Lakini Ofisi hii bado uwezo wake ni mdogo sana, uwezo wa kuweza kufuatilia masuala mbalimbali na hapa naunganisha na suala zima la ujumbe wa Bodi za Mashirika mbalimbali ambayo Mawaziri wanafanya na Mashirika haya yako chini yaani mali zake zinaangaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mawaziri ambao wanateua Wajumbe wa Bodi kwenye Mashirika yetu ya Umma bila Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa na taarifa. Kuna watu wengine ni Wabunge wanahudhuria vikao vya Bodi za Mashirika haya bila kupata maelekezo ya Kiserikali kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina na wakishamaliza kuhudhuria vikao hawapeleki taarifa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Msajili wa Hazina ndiyo inaangalia masuala yote haya. Kwa kweli, tatizo hili limekuwa ni baya sana. Ni baya zaidi kwa sababu kuna baadhi ya watu wanateuliwa kwenye bodi za Wakurugenzi wa Mashirika yetu hawana uwezo, hawana CV ambazo zinaendana na Mashirika hayo na matokeo yao uendeshaji wa hayo Mashirika umekuwa ni mbovu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tuko kwenye Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma taabu tunayoipata ni kubwa mno. Leo tunavyozungumza kuna baadhi ya Mashirika Bodi zimemaliza muda wake mwaka wa nne sasa, mengine mwaka wa tatu sasa hakuna kitu ambacho imefanyika. Madudu ambayo tunayakuta kwenye Mashirika yetu huwezi kuamini kama kuna watu wa Serikali ambao wamo ndani ya Mashirika hayo na mtu pekee ambaye anapaswa kulinda *interest* hizi ni Msajili wa Hazina, Msajili wa Hazina anafanya ni kaidara tu kwenye Ofisi ya Serikali. (*Makofi*)

Namuomba Waziri wa Fedha na nimesema umewahi kuwa Msajili wa Hazina, unajua tatizo hili tushughulikie suala hili tuweze kulimaliza kwa sababu mali tulizonazo kama nchi ni nyingi mno kwenye Mashirika yetu na ni lazima Mashirika haya yaweze kufanya kazi jinsi ambavyo inastahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika taarifa yake ya mwaka huu amesema kwamba kuna suala zima la *conflict of interest* kwa watu ambao ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteuliwa kuingia kwenye Bodi za Mashirika ya Umma, kuna *conflict of interest* na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiye mtu ambaye anatushauri sisi jinsi gani ambavyo Taifa hili linapaswa kwenda. Suala hili limeshafika mpaka kwa Waziri Mkuu tumelifikisha kwa Mheshimiwa Spika, tumelifikisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, tunaomba Serikali ishughulikie suala hili ili wale ambao wanapenda kuitumikia nchi yetu kupitia kwenye Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma waende wakafanye kazi hiyo, watupishe humu Bungeni ili Bungeni wawepo watu ambao wanataka kufanya

kazi ya *oversight* na *legislation*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hilo Serikali iweze kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ina hisa katika Mashirika ambayo watu wengi sana hawafahamu, nitakupa mfano wa shirika moja nalo ni *Celtel* ambayo sasa hivi ni *Zain*. Ni Watanzania wachache sana ambao wanajua kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina hisa 40% katika Kampuni ya Simu ya *Celtel* na Kampuni ya Simu ya *Celtel* imetangaza gawio kwa mara ya kwanza mwaka huu baada ya kelele kelele kuanza na hata hatujui wawakilishi wa Serikali yetu katika Bodi ya Wakurugenzi wa *Celtel* ambayo sasa hivi wanaiita *Zain* na wala hatujui kama taratibu za mabadiliko ya jina na kadhalika na yule mwenye *majority shareholder* alihusisha Bodi ya Wakurugenzi katika Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili nataka nilihu ishe na suala zima la uimarishaji wa soko la hisa Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Stock Exchange*. Nchi zote duniani uchumi wake unapimwa na *capitalisation* katika masoko yao ya hisa, sisi tuna *Dar es Salaam Stock Exchange*, Kenya wana *Nairobi Stock Exchange*, wengine wana *Toronto Stock Exchange* na kadhalika, mpaka dakika hii tunavyozungumza kuna makampuni 11 tu katika Soko la Hisa na tuna makampuni mengi sana ambayo yanafanya faida na mengine ambayo hayafanyi faida kwa sasa lakini yakiwekewa utaratibu mzuri yanaweza yakafanya faida yaweze kuingia katika soko la hisa la Dar es Salaam ili tuwe na *capitalisation* kubwa na ni lazima tujiwekee malengo tuseme itakapofika labda mwaka 2010 tuwe na angalau Mashirika 20 yaliyopo katika soko la hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Nairobi wana takriban Mashirika 35 na ukiangalia unakuta kwamba uchumi unakwenda vizuri sana na uzuri wa Mashirika kuwa katika soko la hisa ni kwamba ni rahisi sana kuweza kupima bei za hisa zinavyopanda na kushuka unaweza ukapima uchumi wa nchi unakwenda namna gani, unaweza ukapima ubora na nguvu ya thamani ya shilingi inakwenda namna gani.

Naomba Serikali iangalie tena kwa *fast track* ni kwa nini 25% katika 40% ya Hisa za Serikali katika *Celtel* zisiende katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, Serikali itapata fedha kwa kuuza hisa hizo hizo lakini vile vile itawawezesha Watanzania wamiliki sehemu ya kampuni hii. Ni kwa nini mpaka leo hii kuna makampuni ambayo yanafanya faida kwa mfano *Tanzania Standard Newspapers* wanafanya faida takriban mwaka wa tano huu mfululizo, tuna hisa 100% kwa nini tusipeleke angalau 30% au hata 25% robo yake kwenye Soko la Hisa? Kwa nini tusiangalie uwezekano wa yale Mashirika kwa mfano *Twiga Bancorp* tuna 100% ya hisa kwa nini tusipeleke kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam? Na Mashirika mengine kadha wa kadha ambayo nimeyaandika katika mchango wa maandishi ili Waziri ajaribu kuyaangalia ili tuweze kuangalia ni jinsi ambavyo tutaimarisha soko letu la hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nyongeza ya hapo *Dar es Salaam Stock Exchange* inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Jengo ambalo wanalifanya kazi juzi juzi ilikuwa Mheshimiwa Rais aende kuzindua ule mpango wa *Enterprise Growth Market* yaani *EGM* matokeo yake ilibidi aende Waziri wa Fedha, isingewezekana Rais

kwenda katika jengo lile kwa sababu ni jengo ambalo lingeweza kumuangukia Rais wetu tukapata matatizo mengine, Waziri akiangukiwa na jengo Rais atamteua Waziri mwingine. Nchi zote duniani kuna zile Wilaya, kuna mitaa ambayo inatumika kwa ajili ya masuala ya fedha, *Dar es Salaam Stock* waliomba majengo fulani, jengo moja lilikuwa la *Railway*, Waziri Mkuu aliyejita Mheshimiwa Fredrick T. Sumaye aliwapatia jengo lile lakini hawakuweza kupewa, lakini kuna jengo ambalo hivi baada ya kuwa Benki Kuu wamemaliza ujenzi wa ile *Twin Towers* na ninashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma juzi *weekend* walikwenda kule Benki Kuu kuangalia ni jinsi gani ujenzi ule umeendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu wote wamehamia katika lile jengo kwa hiyo, yale maeneo ambayo walikuwa wanayatumia kama Ofisi zao kwa mfano kuna jengo la jirani lile jengo wangeweza kupewa *Dar es Salaam Stock Exchange* ili waweze kufanya kazi yao na kuwa karibu na *Central Bank* lakini pia wanaweza kufanya kazi ambazo zinaweza kueleweka kwa sababu tunaziongeza Mashirika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha awasiliane na Gavana wa Benki Kuu waangalie uwezekano kama nilivyosema *under fast track* jengo lile ambalo watu wa *Dar es Salaam Stock Exchange* wameliomba waweze kupatiwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uuzaji wa hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza *Capital Market Authority* na *Dar es Salaam Stock Exchange* kwa kuanzisha *Enterprise Growth Market*, ni nzuri sana na itasaidia sana wawekezaji wadogo wadogo waweze kupata mitaji kupitia soko la hisa. Lakini pia itasaidia Mashirika ambayo hayajafikia wakati wa kupata faida yaweze kuingia kwenye *window* ili yajienteshe vizuri yapate faida na yaingie katika soko kubwa, ni hatua nzuri sana itasaidia sana kuhakikisha *Corperate Governance* katika Mashirika yetu kwa sababu tutakuwa na Mashirika mengi zaidi ambayo yatakuwa katika soko la mitaji na hivyo *Capital Market Authority* na *Dar es Salaam Stock Exchange* wataweza kweli kushiriki katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia pia suala la *unit* pale Wizara ya Fedha ya *Program Support Unity* ambayo inashughulika na masuala ya mahusiano yetu na Jumuiya ya Ulaya kupitia *Cotonou Agreement*. Watu wa Jumuiya ya Ulaya kwa sababu ya haya mambo ya *General Budget Support* wanataka *unit* ile iweze kuvunjwa, ningependa kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwamba tusikubaliane na suala hili kwa sababu bado kuna miradi mingi sana ya kuanzia *EDF8*, *EDF9* na sasa hivi tumeingia kwenye *EDF10* ambayo inapaswa kushughulikiwa na ile Ofisi ya *National Authorising Officer* kwa ajili ya kuhakikisha tu kwamba miradi ile inakuwa inaendana na maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningependa kuishauri Wizara ya Fedha isikubaliane na juhud hizi ambazo hivi sasa maana yake nimesikia *EU* wamesha-*appoint consultant* kwa ajili ya kuangalia uwezekano huo, tutajikuta kwamba muda wote tunawategemea wao kwa ajili ya ushauri na wakati tulikuwa na Ofisi ambayo inaweza ikatusaidia kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hiyo, namuomba Waziri wa Fedha ajaribu kuangalia suala hili la *Program Support Unit* ya mahusiano yetu kuititia kwa *Cotonou Agreement* iweze kuendelea angalau kwa umri wa mkataba ule wa *Cotonou* kwa sababu mkataba wa *Cotonou* utaisha mwaka 2020 na ni eneo hili ambalo linasaidia fedha za *negotiation* zinazoendelea za *Economic Partnership Agreement* kuititia Wizara ya Viwanda na Biashara. (*Makofî*)

Kwa hiyo, tutakapoivunja ina maana kwamba itabidi tuanze kwenda *EU* kuomba fedha kwa ajili ya majadiliano yetu na hao hao *EU*. Kwa hiyo, ni vizuri kwamba tuweze kuendelea kushika eneo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni masuala ambayo nilikuwa nataka kuyazungumzia lakini mengine Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia.

Kwa hiyo, naomba kusisitiza umuhimu wa kuiongezea nguvu kwa kuititia sheria upya ya kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, umuhimu wa kuangalia uboreshaji wa watu amba Serikali inawatuma katika Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika mbalimbali ya Umma ikiwemo *role* ya Msajili wa Hazina kuwa *very clear* kutokana na maelekezo mbalimbali ambayo Serikali imeyatoa. Wasitoke tu Mawaziri na huu ni ushauri tu kwa Mawaziri wajitajihidi kuwa mahusiano ya karibu na Wizara ya Fedha kuititia Ofisi ya Msajili wa Hazina wanapoteua Wakurugenzi katika Mashirika mbalimbali kwa sababu wale kule hawaendi kulinda maslahi ya yule Waziri anayewateua, wanakwenda kulinda maslahi ya Taifa letu, wanakwenda kulinda hisa zetu zilizopo kule. (*Makofî*)

Kwa hiyo, ni muhimu sana kuweza kuhakikisha kwamba watu amba tunawatuma ni watoto wa nchi hii amba wana uelewa na mambo yale wanaweza kutusaidia na Taifa letu likaweza kusonga mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Zitto, nakushukuru kwa mchango wako na sasa namuita Mheshimiwa John Magale Shibuda na Mheshimiwa Mgana I. Msindai ajiandae. (*Makofî*)

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa ili nami niweze kuchangia machache katika hotuba hii ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kwa kutambua kwamba Wizara hii ni mtambuka kwa kushauri yafuatayo, jambo la kwanza kabisa nasikitika kwamba katika Bajeti ya mwaka huu sijasikia mahali popote pale kwamba kutakuwa na manunu ya magari ya kubeba wagonjwa hususani wagonjwa kutoka vijijini. Namshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajaribu kulitazama hili jambo na kwa kutambua kwamba hivi sasa tuna pesa za *EPA* nitashukuru sana kama kiasi kidogo cha pesa za *EPA* zitatumika kununua magari ili tuweze kuboresha huduma ya tiba katika vijiji. Naomba sana suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba iwapo pesa za *EPA* zitakubalika kununua baadhi ya magari, Maswa tunahitaji magari matatu yatakayoweza kupambana na imani ya tiba potofu za jadi kwamba ramli ndiyo *x-ray* na darubini ya kugundua magonjwa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha utusaidie hilo. (*Makofi*)

Kuna jambo lingine ambalo naomba kuikumbusha Serikali, jambo hili ni la kuhusiana na wanafunzi wanaosomea Sheria Chuo Kikuu. Wanafunzi wanaosomea Sheria Chuo Kikuu waliokopeshwa na Serikali wanapomaliza elimu yao ya mabuku wanastahili kwenda kufundishwa kutafsiri elimu ya mabuku kwa vitendo, sasa hawa wanapaswa kulipa tozo la ada maalum ili waweze kwenda katika *internship*. Je, hawa ambao walikuwa ni maskini waliokopeshwa wakamaliza elimu yao sasa wasipokuwa na mfumo wa kupewa pesa za kulipia hizo tozo za ada je, watapata wapi pesa? Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha awe mratibu pamoja na Wizara ya Sheria wakutane na Wizara ya Elimu ya Juu kwa sababu hivi sasa tozo la ada limekuwa ni kikwazo kwa watoto hao kupata pesa za kwenda kulipia ada ili waendelee na *internship*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuikumbusha Wizara ni kuhusiana na utatuzi wa kero za wastaifu. Naomba kuishauri Serikali kwamba ni aibu sana hawa wastaifu walioikopesha nchi hii utumishi wao wanapodai haki zao. Je, inabidi mpaka waende wakatake kulala Ikulu ama inabidi waende kwenye Balozi za nchi za nje, ni aibu sana. Ni aibu na ni fedheha kwa Serikali yetu, ni aibu na fedheha kwa viongozi wetu wa Kitaifa hususani Rais wetu. Naomba jambo hili mkae mjipime, mtafakari na mjaribu kuangalia ni jinsi gani mnawajibika kutatua tatizo hili badala ya kukaa maofisini mkisubiri watu waje, tuwafuate hao wanaolalamika. Kuweni na utafiti wa kujua vyanzo vya migomo hiyo na matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hebu tuijulize na Watanzania wangependa kufahamu hivi ni asilimia ngapi ya migomo inayotokea au utashi wa kufanyika migomo wa walimu, madaktari, wanafunzi huwa na mwelekeo wa chanzo chake kuwa ni mapungufu au udhaifu wa Wizara ya Fedha. Wizara yako ni mtambuka, sasa nashauri Mheshimiwa Waziri ukae vyema ili uwe chachu ya kuhakikisha ya kwamba vyanzo vya migomo, utashi wa migomo wa watumishi na matatizo ya wastaifu sasa uwe umedhibitika kwa kweli myatafutie dawa ili mdai chake asionekane ni mbaya wakati huyo huyo ndiye aliyetukopesha utumishi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba hii ni kweli ni aibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii ya kuwaomba kujitathmini niisititize kwa kusema ya kwamba pana maibuko mengi sana ya malalamiko hata mikoani, lakini Wizara yako ni mtambuka, Waziri una watu mahiri na wenye uwezo na sifa mbalimbali je, ni udhaifu wa eneo gani katika Wizara yako ambao unasababisha hizi kero ziwepo? Wakati pakiibuka malipiko ya kufanya ama kufanyika migomo mnatoa habari za utatuzi wa kero je, Wizara ya Fedha pana mapungufu ya wanahabari wa kuweza kusaidia

kulitaarifu Taifa ili kabla ya malipuko hayo pawe na kuzimwa moto. Rais wetu katuambia kubali kuliwa kidogo ili ule kidogo. (*Makofi*)

Naomba Wizara ya Fedha na Wizara nyingine tuweze kutumia taaluma za wanahabari wa Dar es Salaam, wako wengi sana. Kwa hiyo, ningeomba *Mass Communication* itumike kuwahabarisha wanajamii ili iweze kupata taarifa zilizo sahihi kuliko kuishi kwa taarifa ya vivuli vya ukweli. Ninaomba sana hili mlizingatie. (*Makofi*)

Naomba vile vile, Wizara hii ielewé pamoja na watumishi wote kwamba tupo katika mfumo wa vyama vingi na mfumo wa vyama vingi ni soko la demokrasia ya madomokaya, kwa hiyo, hakuna ujanja wowote ambao Serikali ya CCM hatutaunda shutuma za kuwapa watani zetu pale wakiona pana mapungufu. Watani zetu huvizia hisia za jamii. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukitambua kwamba wewe ni Serikali ya CCM ijithadi kuwatumia wanahabari, naomba sana habari za vivuli na muonekano wa kusadikishwa kwa hodari za uongo uudhibiti kwa kuhakikisha habari zinatolewa kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Nashauri haya kwa kuzingatia ya kwamba mara tu baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais tumekuwa na mazingira tata ya kila mmoja anasema lake analolisema pana maibuko ya fikra potofu huwezi kuyazuia kwa sababu kila binadamu kaumbwa kwa hisia zake na kila hisia ina viwango vyake vya ustaarabu. Tuelewe tuko katika mfumo wa vyama. Hivyo naomba muonekano wa hali halisi utategemea sana watendaji wa Serikali jinsi gani ninyi mnajiimarisha kulinda heshima na sura halisi ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali yake katika kutatta kero za wananchi. Naomba sana Wizara hii ijizatiti kwa sababu ni Wizara mtambuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kutoa shukrani za dhati. Hivi sasa ni lala salama tumekaa hapa kipindi kirefu sana kwa hiyo, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Maswa kumshukuru kwanza Mheshimiwa Spika, kwa huduma zake, kuwashukuru Watumishi wa Bunge wote na pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa mashirikiano mbalimbali yaliyowezesha tukaishi kwa amani na utilivu. Vile vile napenda kuwashukuru Mawaziri wote walioshirikiana nami kwa mawazo ya hali na mali katika kuchochaea ustawi wa hali na mali katika Jimbo la Maswa. (*Makofi*)

Vile vile napenda niwashukuru watumishi wote wa Manispaa wa maeneo mbalimbali ya burudani kwa sababu yangkuwa hayapo maeneo hayo na hawana huruma za huduma basi tungekuwa tunaishi kwa majinamizi. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa huduma zote. Vile vile napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wanahabari wa vyombo vya habari vyote kwa kuelezea habari za Maswa na za Bunge pamoja na nchi yetu. Nawapongeza vile vile wahudumu wote wa mgahawa wa Bunge, ahsante sana kwa huduma zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nasema ahsante sana kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa na fursa ya kukutana na Madiwani wa Maswa walipofika na vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Yusuf Makamba, Katibu Mkuu wa

Chama cha Mapinduzi kwa hafla aliyowaandalia ambayo hajawahi hata kuwaandalialiwa Wajumbe wa Kamati Kuu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Malecela, kwa fursa aliyoleta nayo. Pia nakushukuru wewe kwa huduma nzuri uliyowapatia Madiwani wangu walipokuja Songea, wanakukumbuka kwa wema wako na karibu Maswa, jisikie huru kuja yako au kuja na ndugu na marafiki wengine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, viongozi wenye ukatili wa kujenga saikolojia ya kuikomoa jamii, wawe na subira hususan baada ya hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge hili. Tupo katika mazingira ya mfumo wa Vyama Vingi, tuna uhuru wa kusema lolote, lakini napenda kusema kwamba, kwa sababu tunazungumzia masuala ya fedha na hapa linazungumzwa sana suala la fedha sasa nikutahadharisheni kwamba, Rais Kikwete ni mtu muungwana sana na hapendi ukasuku wa uzushi bila utafiti wa mazalia ya fedheha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kikwete, hapendi majibizano ya jazba ya midomo. Anapenda sana kutumia akili za kufikiri. Kwa hiyo, tuwe na subira ili tuweze kujadiliana kwa uungwana na ustaarabu pale utakapofika wakati wake. Katika awamu ya kwanza, palikuwa na hofu ya nidhamu, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwani anakwenda kama wastara ambaye hapendi kuumbuka, anajenga nidhamu hatua kwa hatua. Awamu ya Nne ni ya makusanyo ya misimu ya Awamu Tatu zilizotangulia, zenye kheri na shari. Kwa hiyo, tumpe fursa na tumuunge mkono sisi Wabunge wote na wa Vyama vyote, watu huwa wanasema, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Tuweni wastaarabu kwa subira na ustaarabu wake ambao ametoa hata uhuru wa kusema yale ambayo ni ya uhodari wa kusadikisha kwa uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsanteni. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye Magalle John Shibuda, nafikiri wote tumemsikia. Nakushukuru Mheshimiwa Shibuda, kwa kutambua huduma niliyowapa Madiwani wako walipokuja kwenye eneo langu la kazi. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Geofrey Weston Zambi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea kuwaita Waheshimiwa Wabunge wanaochangia, sasa hivi nimekuwa nikipokea maombi mapya ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia hoja hii, ambao hawakuleta maombi yao toka siku ya kwanza ya hoja ilipowasilishwa Mezani. Kwa hiyo, naomba niwaambie kwamba, nitaendelea kufuata utaratibu ule wa namna nilivyopokea maombi kwa kuchanganya Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia masuala yote muhimu ya uwepo wao ndani ya Bunge.

Sasa wale walioleta baadaye sana hata kama hawajachangia mara nyingi naomba kusema kwamba, nitawa-*consider* kwa utaratibu nitakaoona unafaa na sio kwa matakwa yao. Kwa hiyo, naomba nitoe tangazo hilo na niendelee na utaratibu nilionao na wao watapata nafasi za kuchangia kwa utaratibu utakaoonekana unafaa na si kwa kuona jinsi

mjadala unavyoendelea Bungeni na namna walivyoona wanaweza kuchangia hoja hii. Maombi yao yamepokelewa lakini yatapangwa kwa utaratibu utakaofaa kwa mwongozo wa Kiti. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hotuba ya Wizara ya Fedha. Naomba nitangulie kwa kuunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wametufikisha mahali ambapo pato letu la Taifa linazidi kukua kwa faida ya Watanzania. Naomba wajitahidi, waongeze spidi na maarifa ili tupate mapato makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuzungumzia *TRA*. Nawapongeza sana, kazi wanayofanya ni nzuri na ni ya kujituma. Naomba uongozi wa *TRA* chini ya Mheshimiwa Waziri wajitahidi kwa mambo yafuatayo: Kwanza, kufanya kazi kwa ubunifu na maarifa zaidi ili kuongeza tija na kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato ya Serikali. Nikizungumzia hapa ni pamoja na misamaha ya kodi; Serikali ipunguze misamaha ya kodi, fedha nyingi zinapotelea kwenye misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ipanue wigo wa kukusanya mapato, bado tuna watu wengi wanaoweza kulipa kodi kwa hiari kama watapewa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwa na uadilifu kwenye utendaji wa kazi na uadilifu kwenye kulipa kodi. Nina imani wafanyakazi wengi wa *TRA* sasa hivi ni waaminifu na wanafanya kazi yao kwa moyo, lakini kuna baadhi ambao wanawachafua wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, tujitahidi kutekeleza kwa dhati Mpango Mkuu wa Tatu (*Cooperative Plan*), tukishayafanya haya, mapato ya nchi yetu yataongezeka na mianya ya kukwepa kodi itakwisha. Watanzania wanapenda sana kuchangia nchi yao, lakini kuna watu wanaowapotosha mpaka wanashindwa kutoa. Kuna watu ambao mpaka leo bado wanawadanganya kuwa watawapunguzia kodi kwa kuwapa kitu kidogo. Kwa hiyo, naomba hilo tuliangalie sana. Mheshimiwa Waziri nina imani yeeye na watendaji wake wote, watafanya kazi kwa moyo safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwa wakulima wa Tanzania. Natoka kwenye mikoa kame na ni mtoto wa mkulima na nikisema mikoa kame ni pamoja na Singida, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Manyara na sehemu ya Arusha, Iringa na kwingineko. Wakulima wetu wadogo wadogo wameshapata mazao ya kuwasaidia ili waondokane na umaskini. Kuna wanaolima alizeti, karanga, ufuta na pamba. Hawa wananchi sasa hivi wanazalisha kwa kiasi kizuri, hali iliyofanya kusiwe na tatizo kubwa la mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hata ukienda kwenye maduka yetu huwezi kukuta kimbo, hata Korie zimepungua kwa sababu mafuta ya alizeti, mawese na karanga, ambayo kwanza ni mazuri kwa afya za binadamu, hayachanganywi na vitu vya ajabu ajabu. Sasa hivi ukienda kote, mafuta haya yapo lakini Serikali inawaonea hawa watu. Nirudi kusema miaka mitatu au minne iliyopita, kwenye Bunge hili hili wakati wa bajeti tulisema, mafuta yanayotoka nje yatozwe ushuru kwa asilimia kumi, lakini mwaka huu wakati wa bajeti Serikali imesema ushuru huo ufutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tulikuwa na kikao cha wawakilishi wa nchi nzima wanaolima haya mazao. Tulifanya hapa hapa Saint Gasper Dodoma na Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake walikuwepo. Wananchi wote walisema ushuru wa asilimia kumi usimame pale pale na walipendekeza iwe asilimia ishirini na Mheshimiwa Waziri ulikuwepo na uliambiwa na washiriki mbalimbali kutoka Tanzania kote kwamba, wanaoagiza mafuta kutoka nje hawaagizi *crude oil*, wanaagiza *semi refine* na yakiingia hapa tutarudi kwenye umaskini. Sasa hivi nenda Iramba Mashariki, Sikonge au kokote vijijini, utakuta mafuta yapo na wananchi wanapata bei nzuri ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokitaka kwa Serikali ni kutuundia Bodi ya Mazao haya; hivi kigugumizi kinatoka wapi mpaka leo? Zamani tulikuwa na *GAPEX* tulikuwa tunakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, naomba asilimia kumi ya kodi ya mafuta isiondolewe na ikiwezekana iongezwe ili wananchi wetu wafaidike kutokana na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani sana na Serikali yetu na imani imekuja zaidi juzi baada ya Mheshimiwa Rais kuzungumza na sisi, lakini bado watumishi wetu wanasumbuliwa. Kuna Wabunge humu humu wanapata pensheni; pensheni zao mpaka leo bado hazijaingia Benki. Sasa kama pensheni ya Mbunge haijaingia; je, mtu anayetoka Kijijini Ibaga kule atafanya nini? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, pensheni za wastaafu wetu ziingie na tulishasema ziongezwe. Tatizo ni nini? Halafu tunasema, mnapotaka kufanya marekebisho waoneni wananchi, wawakilishi wa wananchi tupo humu. Hili la kulipa pensheni kila mwezi halikuletwa humu, lingeletwa humu tungekataa. Kwa nini mtu atoke Kondoa afuate pensheni Dodoma, pensheni yake ni Sh. 50,000, gharama ya kwenda na kurudi peke yake imemaliza hiyo pensheni! Kwa hiyo, kwa niaba ya wafanyakazi wa nchi hii, naomba ule mtindo wa miezi sita sita urudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo ule ulikuwa unawasaidia sana, akipata pensheni ya miezi sita anaweza kufanya kitu kinachoonekana, lakini sasa akija kuchukua hiyo pensheni akirudi nyumbani ni ugomvi na mke wake, anajua huku alishaoa au alikuwa kwenye anasa kumbe pesa yenyewe haitoshi. Kwa hiyo, naomba sana hilo lizingatiwe. Tuna watumishi wetu kwenye Halmashauri zetu za Wilaya; kuna Walimu, Waganga, Maafisa Kilimo na Watumishi wote wa Serikali, kawaida sheria wanatakiwa kupelekewa mshahara kwenye vituo vyao vya kazi, lakini wao wanalazimishwa kufuata mshahara benki na benki ipo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi yule anatumia ghamara kutoka kule anakotoka analipa nauli, anakwenda analala, huyo mtumishi harudishiwi hiyo fedha. Huko ni kuwaonea na kuvunja haki za binadamu; mbona wengine tunafuata mishahara na tunalipwa kwa nini wawe Walimu wa Vijijini, Waganga wa Vijiji? Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo, kama mmeshindwa kumpelekea mtumishi mshahara kule aliko, mlipeni ghamara za kufuata huo mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokubali mwali mu mwingine afuate mshahara, ujue huku kazi zitalala. Jimboni kwangu walimu wanatumia siku nne mpaka tano kufuata mshahara kila mwezi. Sasa ile *syllabus* ya kukosa siku nne au tano kwa kila mwezi, ndiyo inapelekea wanafunzi kushindwa na hii ni kwa nchi nzima. Tunaomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie juu ya kuwawezesha wakulima wetu kupata mikopo. Rais wetu alitamka hapa, zile fedha za *EPA* zitakwenda *TIB* kuwasaidia wananchi wetu wapate mikopo ili waongeze kilimo na kupata tija. Ninachosema, Rais alishasema ile njia ya kuhalalisha hiyo fedha itakuja baadaye, lakini hii shughuli iendelee. Wakulima wetu hata kwa wale ambao wanasema alikosea, wakulima wao bado wanataka mikopo. Rais ametamka hizi fedha ziende *TIB* kama kuna mambo mengine yatafuata baadaye, lakini tumwambie Waziri adumishe *management* ya *TIB* kwa sababu fedha hizi zinazokwenda ni nyingi, ahakikishe bodi iliyopo pale ni imara na itakayowawakilisha Watanzania kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, bado nalia na Wakaguzi wa Ndani. Mpaka leo Wakaguzi wa Ndani kwenye Halmashauri zetu za Wilaya hata huko Mikoani, tunaomba Serikali ichukue jukumu la kuwapeleka shule, kuwatengea kitengo na kuwapa nyenzo za kufanya kazi. Mabilioni ya fedha yanakwenda Wilayani, sasa kama Mkaguzi wa Ndani kila siku atakwenda kuomba kwa Mkurugenzi wake apate usafiri hatutafanikiwa. Kitengo cha Ukaguzi kijitegemee na kipewe nyenzo za kufanya kazi. Wale ni watu muhimu sana na ndio ambao wanatakiwa wagundue mabilioni ya fedha zinazokwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilijibiwa swali langu akasema kwamba, *TRA* itakalofanya ni kuwafundisha vijana wetu wanaokusanya kodi kwenye Halmashauri zetu. Sasa Mheshimiwa amenisaidia sana, sasa hivi kwenye Halmashauri zetu zote tuna wahasibu wenye sifa, wahasibu wenye uwezo ukitoa wachache ambao wamekaa kituo kimoja kwa miaka mingi. Kwanza, hao ambao wamekaa miaka mingi waondolewe, tufuate ile *system* ya kazi, wapewe nyenzo za kufanya kazi na vilevile kama walivyofanya vizuri kuwafundisha wahasibu na Wakaguzi wa Ndani, wafundishwe na watu wa manunuvi wapewe elimu na wapewe vitendea kazi la sivyo tutaendelea na kilio tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri muda bado upo. Sasa hivi niipongeze Serikali, fedha zote za wafadhili zinapita Hazina, kwenye *Basket Fund*, zikitoka pale ndiyo zinakwenda zinapokwenda. Je, fedha za *NGOs* huwa zinapita wapi na zinakuwa *monitored* vipi? Fedha hizi zinatoka Ulaya zinakwenda Vijijini hata miradi inayofanywa

vijijini utakuta hakuna hesabu, miradi ipo Dar es Salaam, Mwanza na Miji mikubwa tu, kule vijijini wananchi hawaoni. Sasa umefika wakati, fedha hizo zote zipite Hazina, tujue zinakwenda wapi na ziwe zinakaguliwa. Kwa sababu zinaingia fedha nyingi, sasa hivi *Global Fund* wanaleta fedha, Bill Clinton analeta fedha, zinapita Hazina na tunazijua; je, za hawa wengine kwa nini zisipite Hazina? Kwa hiyo, naomba sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nazidi kumpungeza Rais wetu amesema, *CDF* ni muhimu kwa Watanzania wa leo. *CDF* ndiyo fedha ambayo itatusaidia sisi kujikomboa katika Kata zetu na vijiji vyetu na kuwasaidia wananchi katika matatizo walijonayo. Hawa wanaopinga hawajui, nina imani wanatumiwa lakini wakija kuona *CDF* inavyofanya kazi, watanyamaza wenyewe na tunaomba kama Rais alivyosema, iunganishwe kwenye sheria hii na ije mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha na Uchumi, lakini naomba niseme kwamba, jina langu ni Godfrey sio Geofrey na sikutegemea Mwenyekiti ukosee jina langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi hayo ni mambo ya kawaida, basi naomba nikuite Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi uchukue nafasi sasa ya kuchangia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naomba nianze kwa kumpungeza Waziri, Manaibu wake na Wataalam wa Wizarani, kwa kuandaa bajeti na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu na kutuwezesha sisi Wabunge kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba niseme tu kwamba, nimeshindwa kujizuia, naomba kama maneno yangu ya utangulizi niseme kwamba, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa hotuba yake nzuri ambayo alikuja kuitoa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Ilikuwa ni hotuba nzuri, ambayo iligusa sekta zote za uchumi wa nchi hii, lakini jambo moja, kwa sababu tunazungumzia Wizara ya Fedha, nilitaka niseme kidogo kuhusu suala la fedha za *EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikra zangu zinanituma kwamba, wale wote waliojihusisha na zile shilingi bilioni mia moja thelathini na tatu ni wezi, ndiyo fikra zangu zinavyonieleza. Hizo bilioni mia moja thelathini na tatu, Mheshimiwa Rais alituambia hapa, ndiyo zilizosababisha Marehemu Balali afukuzwe kazi lakini pia ndiyo pesa hizo hizo ambapo Benki Kuu sasa ipo kwenye mchakato wa kuwafukuza kazi Maafisa waliohusika na upotevu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri pia wale waliojihusisha kughushi nyaraka na kujipatia fedha hizo kinyume na taratibu na wao wawajibishwe. Hakuna sababu ya kuwaonea aibu na kwa kweli nataka niungane na Mheshimiwa Spika alivyosema, hawa

ni sawa na wahujumu uchumi wasiachiwe tu hivi hivi, wachukuliwe hatua zinazostahili.  
(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kuzungumza hilo na kwa sababu lina muda wake baadaye, naomba nizungumze ya kwangu ambayo nilikuwa nimepanga niyazungumze. Jambo la kwanza, ambalo nataka kuanza nalo ni lile la ubinafsishaji na bahati nzuri nilikutana na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkulo, nikamwambia nina mambo yangu ambayo ningependa atakapokuwa ana-*wind up speech* yake, anijibu vizuri kwa sababu ni ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kule Mbozi tuna shamba ambalo zamani lilikuwa chini *NAFCO*; hili shamba lina ekari elfu kumi na mbili na hamsini na moja au hekta elfu nne mia nane sabini na tisa. Shamba hili lilikuwa *specified* kwa ajili ya kubinafsishwa mwaka 1996, leo ni miaka kumi na mbili, shamba hilo bado lipo halijabinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbozi tumeiomba Serikali kwa nyakati tofauti, tangu nimeingia humu Bungeni nimekuwa nalisema jambo hili, aliyekuwa Waziri Mkuu aliyempisha Mheshimiwa Pinda, Mheshimiwa Lowassa, nilizungumza naye na kwa kuandika, lakini pia nimeuliza maswali humu Bungeni ili njue hatma ya shamba lile, lakini majibu wakati wote yamekuwa kwamba, tupo kwenye mchakato, tuliyempata hakuweza, tunafanya *re-evaluation*. Sasa miaka kumi na mbili yote tunafanya *re-evaluation*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Fedha alipokuwa anawasilisha Bajeti ya Serikali, alisema tuna tatizo kubwa la njaa katika nchi hii na njia moja ya kukabiliana na tatizo la chakula katika nchi hii alisema tutachukua hatua zifuatazo na naomba kwa idhini yako ninukuu alisema: “Hاتua muhimu kuliko zote ni kutumia ongezeko la bei ya chakula duniani kama fursa ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini kwa kuhimiza kuwekeza katika mashamba makubwa na kuhimiza wananchi walime chakula kwa wingi ili kujipatia chakula na kipato.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hii, Serikali inatambua kwamba, njia pekee ya kukabiliana na upungufu wa chakula ni kuwekeza kwenye mashamba makubwa. Ardhi iliyopo Mbozi ekari kumi na mbili na hamsini na moja kama zingetumiwa vizuri, nina hakika tungeweza kupata mahindi mengi sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, atueleze vizuri kwa sababu wananchi wale wa vijiji ambavyo vinazunguka shamba hilo, wamekuwa wanaomba shamba hilo, nasi pia kupitia Halmashauri tumejaribu kuomba, lakini Serikali imekuwa haijatusikiliza ipasavyo. Niliwahi pia kuuliza swali humu Bungeni kwamba, Serikali itupe shamba, Serikali ikakataa ikasema *land pressure* kwa Mbozi sio kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba, naijua Mbozi vizuri, *land pressure* iliyopo Mbozi ni zaidi ya asilimia tisini. Kwa hiyo, hii yenye we inatuonyesha kwamba, hata wale wananchi mbali ya kufikiria pengine wawekezaji wakubwa, wangeweza kupewa ardhi ile; nina hakika wana uwezo mkubwa sana wa kuweza kuzalisha chakula na kwa kulisha Mkoa mzima wa Mbeya na kwa maana hiyo, kuweza

kuuza chakula hicho nje ya nchi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, anipe majibu na Wananchi wa Mbozi, hususan Wananchi wa Kata za Isansa, Igamba, Halungu na Itaka, watafarijika sana wakisikia majibu ya Mheshimiwa Waziri kama Serikali imeamua kubinafsisha au itaamua kufanya vinginevyo, lakini kwa manufaa ya wananchi nadhani watafarijika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza jambo hilo, naomba nizungumzie suala la riba ya mikopo kwenye vyombo vya fedha lakini pia hili naomba nimnukuu Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anatoa Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2008/2010 - 2011, alisema riba za mikopo ya benki bado ni kubwa na hivyo kuathiri uwezo wa wajasiriamali kukopa na kufanya biashara yenyе tija na kuwanufaisha walengwa na pia jitihada za kuendelea kupunguza riba hiyo zinaendelea. Naomba Waziri atueleze riba za mabenki zimepungua kutoka wapi na sasa zimefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, naomba pia Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania, kumezuka taasisi nyingi sana za ukopeshaji fedha, nami hizi taasisi nyingine naziona kama ni za kitapeli na ambazo zinawaibia Watanzania. Nimewahi kuzungumza humu Bungeni, nikataja taasisi moja watu wengine wakaninyooshea mikono, kwa sababu hiyo taasisi ilikuwa inamhusu mkubwa mmoja. Hizi taasisi nadhani zinafanya kazi katika mazingira ya nchi za kibepari; katika nchi za kibepari si ajabu kusema kwamba mtu anakula mtu (*man eat man*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taasisi hazijali kwamba huyu tunayemkopesha ataondokana na umaskini au namna gani, wao wanajali faida ambayo wanataka kuipata kwenye mikopo hii. Naomba hapa Mheshimiwa Waziri anieleze. Nitoe tena mfano wa taasisi hizo; kwa mfano, *Bayport Financial Services*, *Blue Financial Services* na kuna taasisi moja inaitwa *Easy Money* na nyingine nyingi. Hebu naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze riba zake hasa kwenye mikopo ni zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizi mtu akikopa shilingi milioni moja anakatwa milioni tatu na laki tatu, kwa miaka mitatu. Mtu anakopa shilingi milioni moja na laki saba, anakatwa shilingi milioni tano. Nilipolizungumza kwa mara ya kwanza, watu walisema nimesema uwongo, lakini baadaye nikatoa vielelezo na ninavyo mpaka leo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hizi ni riba za wapi? Hivi nini kazi ya Benki Kuu, naeleta moja ya kazi za Benki Kuu ni kusimamia benki nyingine na taasisi nyingine? Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri, atueleze hapa hizi taasisi nadhani ni za wizi na naomba nitoe rai kwa Watanzania kuwa, kuendelea kukopa katika taasisi hizi si kujitoa kwenye umaskini lakini tutakuwa tunajidumbukiza zaidi kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunasema, maisha bora kwa Watanzania lakini kwa utaratibu wa kutumia taasisi hizi ambazo Serikali yenye inaziruhusu ziende kukopesha wananchi, halafu wananchi wakienda kule mnasema kwamba wawe makini, kwa kweli haiwezekani. Hawa watu ni wajanja, wanakwenda na lugha walizozitumia akina Karl Peters miaka ile walipokuja kuwadanganya mababu zetu, ndiyo mbinu wanazokwenda nazo, unaweza kupata mkopo

katika muda wa saa mbili au tatu na kwa sababu mikopo katika vyombo vyetu ambavyo ni vya kutumainia hususan mabenki, vinachukua muda mrefu. Mwananchi wa kawaida, anapokwenda akaambwiwa anaweza kupata mkopo kwa muda wa saa mbili anavutika na kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa pale ni kwamba, hawataji *interest*, wana sema *our interest rates are competitive, but how competitive is the interest rate*, hawasemi hapo. Wanasema riba zetu ni za ushindani, lakini ni za ushindani namna gani? Wanasema ukikopa tutakopokuletea mkatiba *then* utaona *interest* zetu, hazina matatizo yoyote, lakini zime watumbukiza Watanzania kwenye matatizo mengi! Kule Mbeya walimu wametumbukia kwenye tatizo hilo kubwa na mimi nina hakika na majirani zangu wananiambia na maeneo mengine mengi. Hebu naomba Serikali tuwasimamie wananchi wetu ili wasiingie kwenye mikopo ambayo hailengi kuwanufaisha zaidi ya kulenga kuwadidimiza katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya sarafu ya shilingi 5, 10, 20, 50 na 100. Kule kwangu Mbozi kuna maeneo wafanyabiashara wameanza kukataa sarafu hizo wakidai kwamba zimeondolewa kwenye mzunguko wa fedha. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi wa kule Mbozi na mahali pengine katika nchi hii, ambapo inawezekana wafanyabiashara wanagoma kuzipokea sarafu hizo kwa kusingizia kwamba zimeondolewa kwenye mzunguko. Nia kama ndio hiyo, wafanyabiashara hao ni kutaka kujinufaisha kwa sababu kama kulikuwa na bidhaa inayonunuliwa shilingi 50 ukiikataa kwamba haitumiki, maana yake unataka kuipandisha bei ile bidhaa bila sababu ya msingi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na hilo uwaeleze wananchi wa kule Mbozi wapate kulielewa, kwa sababu nilishapata tatizo kwenye mikutano ya hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Bima la Taifa ni moja ya Taasisi ambazo huko nyuma ilikuwa ya kutumainiwa sana, lakini miaka kama kumi hivi nakuja hapa mbele Shirika hili lipo kwenye matatizo makubwa sana. Wananchi wengi hususan walimu na watumishi wengine Serikalini, walikata Bima za Elimu na Bima za Maisha na walio wengi, bima zao zilishaiva muda mrefu sana, wengine miaka hata mitano iliyopita mpaka leo hawajalipwa haki zao. Nimesoma kitabu cha bajeti, Mheshimiwa Waziri amesema, mpango ni kulipa madeni mengi inavyowezekana mpaka Desemba 31 mwaka 2008. Naomba Mheshimiwa Waziri, awaeleze vizuri wale ambao wanadai watu ambao waliingia huko kwa matumaini wapate fedha za kuja kusomesha watoto wao, fedha hizi zije kuwasaidia baada ya bima zao kuiva watalipwa lini kwa hakika, kwa sababu ukisema tunalipa zaidi ya asilimia 47, maana yake zaidi ya asilimia 53 zitakuwa hazijalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba, hata wale ambao wanalipwa; wanalipwa kwa ubaguzi. Kuna mtu ambaye alinifuata mimi Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mtu wa Tanga, pamoja na kwamba nina mahusiano naye, lakini anaishi Tanga. Bima yake alikuwa hajalipwa takriban tangu mwaka 2003 au 2004 shilingi 2,000,000 tu. Alipopita kwangu, nikaiwasilisha Bima wakasema kama Mbunge amefuatilia haya, hebu tuifanyie kazi asije akatupeleka mahali pengine. Sasa mpaka ufuatilie Mbunge ndipo wafanye kazi na kweli nilipofuatilia

haikuchukua hata miezi miwili yule mtu akalipwa shilingi 2,000,000 zake na yeye akashukuru kazi ambayo ameifanya miaka mitatu, mine, bila ya mafanikio, lakini tukaifanya kwa miezi miwili. Sijui ni wangapi; kama walivyozungumza wenzangu hapa; hivi Wabunge wangapi tutakwenda kwa Mawaziri tuwafuate au kwa Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma ndipo watu walipwe haki zao?

Haiwezekani kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, awaagize Viongozi wa Bima kwa yale madai ambayo kwa hali yao, wana uwezo ya kuyalipa basi wayalipe kufuatana na yalivyoingia lakini si kwa sababu za kupendeleana au kwa sababu pengine ya kutaka wapate kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo, mengine niliyoyazungumza nilikuwa nimeshayaandika na Mheshimiwa Waziri alikuwa nayo, nilitaka tu niyazungumze Watanzania wayasikie na pia wamsikie Mheshimiwa Waziri akiyajibu. Mimi nilisema kwenye mchango wangu wa maandishi, sitaunga mkono hoja mpaka Waziri anieleze hususan suala kubwa kwangu ni Shamba la NAFCO Magamba. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo ya kuridhisha na ndipo nitakapounga mkono, lakini kwa sasa naomba niseme tu kwamba, sitaiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITU:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Faustine Kabuzi ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa zawadi ya uhai na pia nashukuru jinsi ambavyo leo ameweza kuifanikisha siku hii. Naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wetu wa Fedha, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Tumepokea hotuba hapa nzuri, yenye kuleta matumaini japo mambo mengine yaliyozungumzwa mwaka jana hayakujitokeza tena, lakini kwa vile mara nyingi yanaulizwa kwenye maswali, basi tutaendelea kujua mambo yatakavyokuwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa na kabla sijaendelea kuchangia hoja hii, naomba nitoe pole kwa wale Wanafunzi wa Machame Sekondari na wale wa Bigwa Sekondari, waliopata tabu katika maafa ya moto hivi karibuni. Inaleta tabu na inatia wasiwasi, inaonekana kama yale mambo ya majanga ya moto katika Shule za Sekondari yanajirudia tena. Baadhi ya shule hizo ikiwemo Machame haina uzio, ningemba tu jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuzungumzia kwenye suala la kushughulikia uwekezaji kwenye hisa. Shughuli ya hisa au uwekezaji kwenye hisa ni jambo zuri na hata ukilinganisha gawio linalopatikana kwenye hisa, linazidi ile riba inayolipwa na Mabenki. Pamoja na kwamba, Tanzania ina nia nzuri ikiwemo Serikali kwamba, wananchi wawekeze kwenye hisa, elimu ni kidogo sana kwa wananchi wetu. Sasa hapa

nauliza; Waziri amejiandaaje pamoja na hizo taasisi za fedha zinazouza hisa, kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi?

Hadi kufikia leo ni Benki moja tu ya CRDB, ambayo huwa inatoa elimu kwa wanahisa wake kila mwaka na kila mwezi Aprili lazima kunakuwa na semina ya wanahisa. Jambo hili ni zuri na wanahisa wa CRDB wanajua kwamba, ongezeko litakuwepo mwezi Juni. Nichukue fursa hii, kuwapongeza sana kwa gawio zuri tulilopewa wanahisa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajiandaa kununua hisa za NMB, tumefika pale kwenye Ofisi za NMB hatujapewa hizo *prospectors*. Hatujui manufaa yatakuwaje na pia ni lini basi jambo hilo tutaona limefanikiwa, *break even point* itakuwa lini. Sisi tunakwenda tu kichwakichwa hisa za NMB kwa vile NMB ina mtandao kila mahali tununue. Je, ni lini sasa hisa hizo zitaanza kulipwa, bado hatujapatiwa elimu hiyo wala vipeperushi? Mimi jambo hili linanishangaza sana; tunaomba tupatiwe elimu ya kutosha, tupatiwe vipeperushi na pia vitabu nya kueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba, soko la hisa lipo Dar es Salaam. Sasa huku mikoani mwananchi wa kawaida hapati kwa urahisi, pale anapotaka kutoa hisa yake igeuke kuwa fedha, inabidi aanze kuuliza uliza; hivi kweli kama Serikali ina nia kabisa sisi watu tuwe na hisa na tuwe maarufu kama walivyo Kenya wenzetu wanavyokuwa na hisa kwenye kila Kampuni; kwa nini jambo hili lisitiliwe mkazo watu wakaelimika kisawasawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni jambo ambalo sio endelevu, ikiwa wanahisa au watu wanaonunua hisa, wanaziweka tu ndani ili mradi wawe wanapata gawio kila mwaka. Ili uweze kufaidi hisa ni kununua hisa zikiongezeka bei, unaziuba yaani *undispose* labda unanunua tena hisa za Kampuni nyingine. Nilikuwa naomba sana Serikali itoe elimu na pia iwasiliane na hizo taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba kuzungumzia SACCOS, hapa wengi wamezungumza kuhusu riba kubwa kwenye mikopo inayotolewa kila mahali zikiwemo pia hizi *Savings and Credits Scheme*. Ninachotaka kuzungumza hapa sio ule ukubwa wa riba ambayo wanatozwa wale wanaokopeshwa, mimi hapa nataka kuzungumzia riba ndogo ambayo mtu anayeweke fedha yake Benki analipwa. Nilizungumza tena wakati ule kwenye Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, lakini sasa narudia tena; hivi kweli Serikali imeshindwa kabisa kuzungumza na hizo taasisi za fedha ili watu wapate motisha kwa kulipwa *interests rate* kubwa angalau hata mbili juu ya hii inayotolewa sasa ikawa asilimia 3, 4,5 ili watu wapate msukumo wa kuweka fedha yao Benki? Jambo hili linanishangaza kabisa. Tunaambiwa kwamba ni biashara huria, hata kama ikiwa biashara huria, kazi ya Benki Kuu ni nini? Si kusimamia! Tunaomba tuone hiyo kazi ya Benki Kuu sasa ikizungumza mezani na hizo taasisi tupate changamoto ya kwenda kuwekeza kwenye Mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hiyo ya *Savings Interest Rate*, naomba nizungumzie juu ya asasi za mafunzo hapa nchini; nyingi zimetajwa kwenye

Kitabu cha Waziri, lakini naomba nizungumzie tu asasi moja ambayo inanipa woga. IFM ni Chuo kizuri sana, kimeendelea kupata wanafunzi mwaka hadi mwaka, lakini hali ya kimaisha ni mbaya sana. Kila leo wanafunzi wanaongezeka, bila uongozi kujali wale wanafunzi wanaishi wapi. IFM ipo katikati ya mji, wale wanafunzi wanaishi kwa shida sana, namna ambavyo vyumba vile vile vilivyokuwa vinapokea wanafunzi 500 sasa hivi vinapokea wanafunzi 4,000 na kuendelea. Sasa tuijulize, hivi hawa vijana wetu wanaishi wapi? Unakuta chumba kimoja wanaishi hata vijana wanane kwa kupokezana kwa saa. Mimi bwana nikienda kusoma darasani wewe ulale kidogo, ukiamka wewe unakwenda kusoma mimi nakuja kupumzika; hivi kweli kwa namna hiyo tutafika?

Mimi nilikuwa naona chuo hiki kwa vile ni mfano na kipo mahali pazuri kabisa, ijengwe sasa hosteli nje ya pale lakini iwe ni hosteli kwa wanafunzi wa IFM. Kati ya wanafunzi ambao wana shida nchi hii, mimi nakiri kwamba wanafunzi wa IFM wanaongoza. Naomba Serikali ilitupie jicho suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia lipo katika ukurasa wa 43, nalo ni juu ya mfumo wa malipo kwa mtandao (*E-payment System*). Mimi nichukue nafasi hii, kuipongeza sana Wizara kwa kuliona hilo. Mara nyingi Wafanyakazi wa Serikali walikuwa wanapata matatizo; mishahara inaibiwa wakati ambapo inapelekwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Imekuwa ni shida ambayo ni endelevu. Sasa naona ufumbuzi umepatikana na hapa naomba niipongeze sana Wizara kwa kuliona hilo. Kwamba, wanasema malipo haya yatafanyika Benki Kuu na Wizara ya Fedha, katika utaratibu wa ulipwaji zitahamishwa moja kwa moja katika akaunti yake kutoka akaunti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu: “Utaratibu huu utakapoanza, wote wanaolipwa au wanaofanya biashara na Serikali, watalazimika kuwa na akaunti za Benki. Ina maana basi wakati wa malipo, fedha za hao wanaolipwa zitaingizwa moja kwa moja katika akaunti zao.” Sasa hapa nina maswali mawili; katika kuanza mfumo huu Serikali imojiandaa vipi na wizi kwenye mtandao? Wizi wa mtandao ni mbaya kuliko ule wizi wa kughushi kwa kalamu. Maana huku ndiko zinakoibviwa fedha nyingi, anayemjua mtu wake kwenye *system* zinajaziwa fedha huko ili mradi anarundikiwa fedha lukuki. Mimi nasita, lakini nadhani ni ukweli haijatungwa sheria ya wizi kwenye mtandao. Hii ni tofauti kabisa na ile ambayo mtu utakuta amechorachora halafu *ka-forge signature* au utakuta maandishi. Hii haitakuwa na maandishi ni *block* ya fedha au *amount* ya fedha *then* itakuwa na *list* itaingizwa huku; je, wizi huo tutaudhibiti vipi? Nilikuwa naomba Wizara iliangalie jambo hilo ili kama inawezekana, basi Sheria ya Wizi itungwe kwenye mtandao mara moja na adhabu yake iwe kubwa zaidi kwa sababu unaweza ukafanyika wizi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukwepa hilo sasa hivi, mambo ya kupeana shilingi kwenda kusimama mbele una foleni kulipwa hundi yamepitwa na wakati, ni kiasi tu cha watu wapewe *instruction* fedha hizo ziingizwe. Wizi huu kama nilivyo sema hapo awali ni mbaya sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuangalie hayo na inapobidi basi, tuweze kusaidia kudhibiti kwa sababu huko kutakuwa hakuna kunyoosheana kidole kwamba, umesaini wewe au amesaini yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya kusema hayo yote, niseme tu kwamba, katika hotuba ya mwaka jana wakati Wizara haijaunganishwa ilipokuwa ni Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, tulielezwa kwamba, yatatolewa mafunzo kila mkaoa kwa wajasiriamali ili wajue kubuni miradi yao wenyewe. Kule Kilimanjaro, tumeyasubiri sana mafunzo mpaka sasa hayajafika. Mimi naona au niamini tu kwamba, mafunzo hayo yanakwenda kimkoa kwa awamu. Niiombe Serikali sasa kwamba, uwe ni wakati muafaka na wale Wanawake wa Kilimanjaro waletewe mafunzo hayo ili tujue sasa jinsi gani miradi iandikwe na jinsi gani ipelekwe kupatiwa fedha Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naamini kwamba, Wizara itazingatia hayo. Naomba kwa heshima niunge mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Shally Raymond kwa mchangwo. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir ajiandae na nadhani atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie. Nashukuru kwa wema wako, wewe ni mwema daima na tulipotembelea jimbo lako ulikuwa mwema na ultukarimu vizuri sana. Nashukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuipongeza Wizara ya Fedha; inafanya kazi kubwa na ndio imetufanya kipindi chote hiki tuwe hapa na leo yenyewe inaomba fedha. Sisi sote tunaitegemea na ina wajibu mkubwa kwa nchi nzima, bila Wizara hii nadhani tusingekuwa hapa.

Napenda nianze na kuiomba, pamoja na kwamba leo tupo kwenye hatua za mwisho, tunagawana kila mmoja amepata kasungura, tumepata angalau mgao umekuwa mzuri, lakini wasiwasi wangu ni katika utekelezaji baada ya kutugawia mikoa na wilaya. Ukiangalia taarifa za *Auditor General* za miaka iliyopita, zinasikitisha sana na hatua zilizochukuliwa zinaonyesha kwamba hatujaweka mkakati wa kuwaumiza au kuhakikisha kwamba, watu wanaogopa fedha za umma, wananchi wetu wanatutegemea sana. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna haja na napenda kuuliza ni mkoa upi kwa sababu kila mkaoa, kila wilaya na kila Wizara, kuna fedha ambazo zinaonekana hazikutumika vizuri; ni hatua zipi zimechukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza na mwenzangu hapa tufanye nini ili tuweze kuondokana na tatizo hili. Nadhani kuna mahali tuna haja ya kuweka mamlaka kwamba, mtu kama amekosea hakuna sababu ya kusema kwamba, karatasi hazijapatikana sijui vitu gani havijaonekana kwenye *document*, kila mmoja awe navyo ili tuwe waaminifu katika hili na hili limejitokeza hata katika fedha nyingi zinazoibowi. Tunakusanya fedha kwa kubembeleza watu na kwa sababu tuliondoa ile nguvu ya Serikali hata kum-*detain* mtu kama anaharibu. Mimi natoka Geita karibu na mgodi; wakikuona una mashaka mashaka wanakufukuza na wanakuchukulia hatua kwamba una

dalili za wizi. Sasa hawa watu ni vigumu sana kuwakamata kwa sababu ukimpeleka Mahakamani mtu mwenye fedha si rahisi kumshinda. Sasa kama si rahisi kumshinda, maana yake kama hawa watu wataendelea kuiba, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuanza kufikiria kama tutaendelea hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanza Bunge hili, Rais aliita semina elekezi kwa Mawaziri na kwa Wakuu wa Mikoa, nikatarajia sasa Mawaziri na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, hiyo semina elekezi watakwendwa kuifanyia kazi. Ukiangalia kwa sehemu kubwa ni kama alikuwa anapoteza muda. Sasa nilikuwa nasema; je, hizi semina tuendelee nazo tu? Maana ya semina elekezi sio kwenda kula fedha ni kwamba, tunatakiwa tuwajibike kwa wananchi na fedha tuzitumie vizuri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba tutakapokutana tena mwakani, tusingependa kuona fedha nyingi kama hizi zilizopotea. Tuna matatizo mengi, wananchi wanahangaika, wanateseka na hatuwezi kusema kwamba nchi yetu haina fedha. Ina fedha nyingi za kutosha na tunaweza kuzikusanya tukazidi nchi nyingi ambazo nadhani tuige hata mifano ya nchi jirani kama Rwanda. Rwanda anakuita anakunyofoa na anakwambia nakuweka ndani anakushughulikia. Kwa hiyo, kila mmoja anaogopa hata ukidondosha pochi jamaa anakwambia pochi yako hii hapa, lakini sisi kwetu hakuna. Nadhani tunahitaji kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo mengi, sasa hivi tuna malimbikizo ya walimu, walimu hawa tumeshindwa kuwalipa. Mimi sisemi waongezwe mshahara, lakini kile kidogo chao kwa mfano, kwenda likizo, matibabu na mambo mbalimbali tuwape. Sasa hii mianya inafanya hata tushindwe kuwalipa, Mwalimu anateseka anafanya kazi kwa mshahara mdogo. Kuna Wilaya nyingine utakuta kweli zimelipa vizuri, lakini nyingine zinashindwa kulipa, ina maana kuna Wilaya inapendelewa, sio zote zinapewa fedha sawa. Serikali inatoa fedha vizuri tu mwingine hapeleki, unakuta kuna wajanja, kila mmoja anataka kununua gari, anataka kujenga nyumba haraka; jamani hawa watu watazamwe kuna watumishi wanahangaika. Kuna Polisi tunawatumwa bila hata kuwapa posho zao; je, ni kweli kwamba tunashindwa kiasi hicho? Tunahitaji kuwa wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la watumishi wanaposafiri kufuata mishahara yao; kwa mfano, kwangu kuna walimu wanatoka Bukondo kwenda kufuata mshahara Geita. Anatoka Nyambalimbe kwenda kufuata mshahara Geita ni mbali sana na anakaa siku mbili, tatu, hawezi kupewa hata fedha ya kusaidiwa kutoka hapo. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, miaka ijayo tuwawekee nyongeza, kwa sababu mshahara akianza kuula kule akirudi nyumbani ni matatizo matupu; mshahara ni mdogo anaanza kuutumia kule na hata watendaji wa vijiji vile vile. Humo ndani kuna haja ya kuangalia; je, tuna maumivu kiasi ambacho hatuwezi kukusanya fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani *TRA* inaweza kukusanya zaidi juu ya hizi tunazofanya na hakuna sababu ya *TRA* kufanya kazi kwenye maeneo kwa mfano ya Bandari saa nane wanaweza kufanya saa 24. Waende Mombasa wakaingalie Bandari ya Mombasa; kwa nini watu wanakimbia hapa wanakwenda Mombasa na bandari nyingine? Tunaweza kuzalisha hapa. Kwa hiyo, wao Jumapili na Jumamosi wanapumzika hapa na watu wa bandari wanapumzika wakati kuna mizigo pale; kwa nini tusifanye saa 24 watu;

wafanye kazi hata kwa *shift* wasafirishe mizigo, lakini wanapumzika wanamzungumsha mtu mpaka atoe chochote ndio mzigo utoke? Nadhani tunahitaji kubadilisha tabia na mila zetu tuweze kufanya kazi. Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba tuliangalie.

Suala la pensheni tumelalamika sana, watu wanaostaafu wanateseka. Ndugu zangu sasa hivi tunafikia mwaka 2010, wengine tunastaafu na wengine bahati nzuri wataendelea, lakini utakapostaaafu ndio uthaona uchungu wa kustaafu. Kwanza, unastaafu uko kwenye umri ambao huna uwezo unategemea hiyo fedha sasa inakaa miezi mitatu; kwa nini kusiwe na rekodi? Tumesema kuwe na rekodi, mtu apewe fedha zake asihangaike. Mirathi hivyo hivyo, lakini watu wanawazungusha wanahangaika, ukifika wanaopanga foleni pale Wizara ya Fedha zunguka kule nyuma angalia waliokaa pale wote wamechoka wanakuja kwa nguvu ya Mungu, roho ipo juu juu hali mbaya. Nilikuwa nadhani kuna haja ya Mheshimiwa kuanza kuangalia; je, ni vipi hatuwezi kujisahihisha? Nadhani Mheshimiwa Waziri, tunakutegemea sana, hatupendi kusikia fedha za wananchi zinatumika ovyo. Kuna fedha zimepelekwa sana kwenye Wilaya, lakini mtu asije kusema *documents* hazijaonekana, tulikuwa hatujawasilisha wewe unapenda kula hutaki kuwahisha *documents* lazima tuwe wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzetu amezungumza, kwenye Bodi na kwenye Mashirika ya Umma nako kuna matatizo makubwa sana. Amezungumza tatizo kubwa ni *u-conflict of interest*, Wabunge hao ni Wajumbe wa Bodi. Nakubaliana naye kitu kimoja tu kwamba, Mbunge kama hana uwezo kwenye eneo hilo, hakuna sababu ya kumuweka. Wabunge humu mimi nasema wana akili na wanaweza kuchanganyika ni Wachumi. Huwezi kuniambia mimi nitoke nje nikulindie mji wako, mimi natakiwa niwe humo humo niangalie nitoe taarifa kwa Serikali, labda kama sielewi jukumu langu. Kama Mbunge yupo kwenye Bodi, anatakiwa atoe ripoti na aangalie kama ni wa kwanza kutoa taarifa. Huwezi ukamwambia akae nje halafu sheria zinakwenda. Yeye ni mwakilishi wa Bunge, mwakilishi wa Serikali na wa wananchi, akiona hapa kuna tatizo hawezi kukaa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe una mji wako umwachie mtu akulindie familia yako halafu unasema nini! Kama tunasema Makatibu Wakuu au Wakurugenzi wawemo humo, basi kinachokufanya uogope kumdhhibit Katibu Mkuu, ndio hicho hicho kinachofanya uogope kumdhhibit Mbunge. Katibu Mkuu na Mbunge kuna tofauti gani? Mbunge kama hatimizi wajibu wake si wanaleta hapa kama yupo kwenye Bodi au anawajibishwa; bwana hukutumiza wajibu wako anateuliwa mwingine. Mjumbe wa Bodi si Ubunge ni kwenda kufanya kazi kama watu wengine. Yule anayesema naogopa Wabunge hawezi kazi aondolewe. Mimi nasema na namwambia kama utawaondoa Wabunge, umetoa jicho lako kule yaani umewaachia watu mambo yaende kienyeji, hapo utapata tabu. Angalia sana, ushauri mwingine mzuri lakini kweli mtu awe na uwezo. Sio mtu aende pale kucheka cheka, kufanya nini anaondoka na posho, hapana. Anakwenda kule na uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri; hizi fedha tunazogawana ziwafikie wananchi. Watu hawana maji na tunaomba Mheshimiwa Waziri, jicho lako lipo kwenye eneo la

madini; hebu hamishia jicho kwenye eneo la madini tuwe kama wenzetu wa Botswana. Mshauri Rais, jicho lake lihamie kwenye madini; tuna uwezo mkubwa sana hapa nchini. Usiende kilaini laini, pale wale ni wafanyabiashara wanataka faida na sasa hivi tunavyozidi kuwapa nafasi kutolijadili hili suala wanazidi kuongeza mitambo na kuchimba kwa nguvu na tutaishia makombo, sisi tunawaona kule wanavyofanya kazi saa 24 wakati tunakwenda kulala wao wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabuzi, naomba tu kusema ule wema unaofanyika kule kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea ni kwa sababu tu Wananchi wa Jimbo la Peramiho ni wananchi wenyewe ukarimu sana na ni wananchi wachapakazi na ndio maana wengi mnakuja kujifunza katika Jimbo langu la Peramiho. Naamini tutasaidia wengi ili kuendana pamoja kama vile tunavyofanya ndani ya Jimbo letu. Nakushukuru Mheshimiwa Kabuzi.

Waheshimiwa Wabunge, nimesema mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Zubeir Ngwali Maulid, naomba nimwite. Mheshimiwa Zubeir karibu.

**MZEE NGWALI ZUBERI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasahihisha jina langu sio Maulid naitwa Mzee Ngwali Zubeir.

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa Ngwali Zubeir.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawashukuru Mawaziri wa Wizara ya Fedha, kwa hotuba yao nzuri waliyoitoa tokea juzi. Pia naishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hotuba yao nzuri waliyoitoa juzi hapa Bungeni. Nataka kulizungumzia suala zima la *Special Economic Zone* iliyoko Mabibo na muda mwangi nitapoteza kuzungumzia suala hilo. Kuunganishwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango, kunaonekana kuwa kama Wizara ya Mipango bado haijaimarika zaidi. Lkini kama itaundwa Tume ya Mipango, ikiwa inajitegemea basi itakuwa ni vizuri zaidi kwa sababu hivi sasa Tume ya Mipango kama itafanya kazi vizuri basi matatizo mengi yanaweza yakajitokeza kuhusu mipango yetu tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima ambalo ninataka kulizungumzia ambalo ni *Special Economic Zone* ya Benjamin William Mkapa, iliyopo Mabibo, imeanza tangu mwaka 2005, lakini mpaka hivi sasa Wizara ya Fedha bado haijawa *serious* na lile eneo kuhakikisha kwamba, linafanya kazi. Hivi sasa Mradi ule unahitaji kama shilingi bilioni 40 ambazo zitasaidia kuukamilisha na kufanya kazi zake vizuri. Kikwazo kilichopo pale ni kutokupatikana kwa fedha hizo na Mradi bado haujawa endelevu mpaka hivi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo linazungumzwa wakati huu tulionao ni kuhakikisha tunawekeza katika sehemu mbalimbali kwenye Mikoa yetu. Mpaka sasa

tatizo linalokabili eneo hili ni fedha na ambalo ni tatizo sugu. Jambo la haraka ambalo linahitajika ni kuhakikisha kuwa, wanafidia wakazi wa pale ambao wanahitaji kiasi kama cha bilioni mbili. Ununuzi wa magari ya Zimamoto utagharimu kiasi cha bilioni 2.5. Ununuzi wa vifaa vya ujenzi utagharibu shilingi bilioni 2. Kituo cha Umeme cha kujitegemea kinahitaji shilingi bilioni 6.3. Ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama barabara na mingineyo unahitaji sgilingi bilioni 4.3. Mfumo wa Majitaka unahitaji shilingi bilioni 1.2 na ukarabati wa majengo na ofisi unahitaji shilingi milioni 200. Kwa hiyo, tatizo lililopo pale huku mradi ukiendelea ulikadiriwa kukamilika mwaka 2007, lakini mpaka hivi sasa bado haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo yafuatayo: Kwanza, tuhakikishe kuwa eneo lile linapatiwa fedha ya kumalizia ile miradi. Kwa sababu fedha walizopata mpaka hivi sasa hazizidi shilingi milioni 23. Kwa hiyo, wakiongezewa fedha na kumalizia ule Mradi, unaweza ukazalisha ajira nyingi pale kwa vijana wetu zisizopungua milioni 2 mpaka milioni 3. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie ile hela ambayo inaweza ikapatikana ili kukamilisha mradi ule zipatikane na kuhakikisha kuwa eneo lile linaweza likafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ule uzio ambao tayari umeshajengwa, lakini zile nyumba za jirani wanatakiwa wafidiwe na kama nilivyosema zinahitajika shilingi bilioni sita ili kuhakikisha usalama wa eneo lile unapatikana. Kwa hiyo, fedha hizi zikipatikana, wanawenza wale wananchi wakahamishwa pale na eneo lile likanza kufanya kazi. Sasa suala ambalo lipo pale ni kuhakikisha kuwa, lile eneo kwa muda huu tulionao, tayari sehemu nyingine zinaweza zikafanya kazi na maombi yameshapelekwa, wamejitokeza wawekezaji wasiopungua 50 wameshaomba.

Sasa kama Wizara inahakikisha kuwa, wameshaomba na wanaweza kufanya kazi, naomba Mheshimiwa Waziri alione hili ili wawekezaji waweze kufanya kazi au maombi yao yaanze kufanya kazi kwenye lile eneo. Kwa sababu kama tutasubiri mpaka limalizike na ufinyu huu wa bajeti tulionao, haliwezi kukamilika kwa kila kitu. Kama litakuwa limeshaanza kufanya kazi, mambo mengine yatakuwa yanaendelea katika utaratibu unaostahili.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri; Wizara ya Fedha iliangalie lile eneo. Tusiachie hapo tu, tuhakikishe kwamba, tuna malengo ya muda mrefu na kuhakikisha kila Mkoa unapata uwekezaji, lakini uwekezaji tulionao mpaka hivi sasa katika maeneo haya ya SEZ ni moja na lingine linataka kuanza Kibaha sijui ni mwakani au mwaka unaokuja. Tuna mtarajio ya miradi kama hii isiyopungua 25 mpaka 30 kwa nchi nzima, lakini bado mpaka hivi sasa tunasusua, tuna mradi mmoja tu ambao umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tujitahidi katika hali hii kuhakikisha kuwa, uwekezaji wetu au mipango yetu na fedha inapatikana tuhakikishe tunaendelea na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu suala la Chuo cha Mipango Dodoma. Mheshimiwa Nyawazwa kaligusia kidogo. Chuo hiki hivi sasa kinapiga hatua kweli kweli na wanafanya mambo mazuri tu, lakini kuna suala zima la walimu wa muda (*part time teachers*), wapo wengi sana pale. Tuwasaidie waondokane na suala hili. Kwa hiyo, wale walimu basi waajiriwe ili walimu waajiriwa wawe wengi zaidi kuliko *part time teachers*, kwa sababu ni suala la kupoteza fedha nyingi lakini manufaa yake yanakuwa madogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine; kwa nini Chuo cha Mipango kiwepo Dodoma peke yake kisianzishe matawi sehemu nyingine; basi angalau tuenze kwa kanda, kwa mfano, kanda ya mashariki, kanda ya ziwa, kanda ya magharibi na nyingine? Tukianzisha matawi kwenye kanda hizi, itasaidia sana. Vilevile tuhakikishe walimu waliopo pale wanapatiwa nyumba au makazi maalum ya kudumu. Kwa sasa hivi wanatumia fedha nyingi kwa sababu ya usafiri na usafiri wenyewe haupo na huo uliopo wanatumia mafuta mengi. Kwa hiyo, kama wanapata nyumba za kudumu pale, basi ingesaidia sana walimu waliopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine ambalo napenda kulizungumzia kuhusu *TRA*. Kati ya watu ambao unaweza kuwatolea mfano Tanzania ni *TRA*, kwa sababu wamefanikiwa sana kwa hatua ambazo wanazipiga hivi sasa. Kwa kweli ni kitu cha kupigiwa mfano na cha kuigwa katika taasisi nyingine. Suala ambalo nataka kulizungumzia kwa *TRA* ni kuhakikisha kwamba, wanaleta ufanisi zaidi na wanafikia malengo yao. Kwanza, kama mlivyosema, wanakunsanya kodi nyingi nchini na inasaidia sana. Tatizo lililopo ni katika kuongeza mapato yetu, sehemu za mipakani bado hatujawa waangalifu sana kuhusu ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza kuidhibiti mipasuko au njia za panya zilizoko katika maeneo ya mipakani, basi ongezeko la fedha linaweza likapatikana. Hata hivyo, mazingira yaliyopo katika maeneo yale, tukiyaboresha itakuwa ni vizuri zaidi, kwa sababu si mazuri. Tumetembelea Hororo tumeona hali halisi, kile kichochoro wanachofanya kazi *TRA* hakipendezi. Nawasifu sana, hivi sasa kuanzisha jengo zuri Babati, ambalo tayari wameshaweka msingi na linaendelea vizuri. Kwa hiyo ni vyema kuhakikisha kwamba, kwenye mipaka yetu mapato yanapatikana ipasavyo na yale majengo tunayaboresha.

Si hayo tu, majengo ya *TRA* hata majengo mengine, ukiangalia utaratibu mzima au mfumo mzima wa uendeshaji wa Wizara zetu mipakani inakuwa ni mbovu. Ukiangalia Vituo vya Polisi haviridhishi, Uhamiaji hakuridhishi na hiyo *TRA* hairidhishi. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa haya mambo yaliyopo, kuhakikisha tunaweka mazingira mazuri na yanafanya kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Benki Kuu. Benki Kuu, ina majukumu yafuatayo: Usimamizi wa Fedha na Sera za Fedha, usimamizi wa Vyombo vya Fedha, utoaji wa sarafu, usimamizi wa Mabenki ya Serikali na ya Biashara. Haya ndiyo majukumu yake, lakini tatizo sugu lililopo hivi sasa ni kutowaelimisha wananchi kuhusu fedha bandia. Nilifarijika sana nilipoona maonyesho na wale wataalam jinsi wanavyoelimisha kuhusu fedha bandia kwa wananchi. Wanaelimisha sawa, lakini elimu

ile isiishie kwenye maonyesho tu. Hata wananchi wa kawaida, wanapoteza fedha zao kwa sababu hawazielewi noti zile bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nashukuru kwa Benki Kuu ni kutoa taarifa kila baada ya muda na kama walivyojiwekea, Gavana wa Benki anasema kila baada ya miezi mitatu watatoa taarifa ya hali ya uchumi na hali ya maendeleo ya uchumi wetu tulionao. Suala hili liendelee kwa wananchi wote na wahakikishe wanatoa elimu kuhusu maendeleo yao ya uchumi jinsi unavyokwenda. Vilevile Benki Kuu inasimamia Taasisi za Fedha, lakini tatizo *ATM* zetu zilizopo Tanzania ni tatizo. Wanakwambia saa 24 kufanya kazi, lakini kumbe kero yao ni saa 24, yaani ile kero ya *ATM* ni saa 24. Kwa hiyo, lazima Benki Kuu iliangular hili ilisimamie kuhakikisha kuwa zinafanya kazi saa 24 na hazileti kero ya saa 24. Usiende pale ukakuta *ATM* haifanyi kazi. Kwa hiyo, naomba lihakikishwe hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni *PPF*. Mfuko huu unafanya kazi nzuri, kama aliavyoeleza Mheshimiwa Waziri kwenye Hotuba yake. Suala zima ambalo linaikabiri Mifuko yote Tanzania kwanza ni Ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa huu unaisumbua Mifuko yetu na lazima suala hili tuwaelimishe wafanyakazi wetu kwamba, gonjwa hili lipo na wachukue tahadhari ipasavyo, kwa sababu Mifuko inaweza ikala hasara kwa kulipa fidia kubwa kuhusu magonjwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu uwekezaji wa nyumba za wapangaji. Mifuko yetu kama hawatakuwa waangalifu, siku zote watakuwa wanapelekwa mahakamani. Kwa sababu inaonyesha kuwa, Sheria zao au Mikataba yao inakuwa hairidhishi. Kwa hiyo, lazima wawe waangalifu kwa watu amba wanawapangisha waweke sheria na mikataba mizuri ya kuhakikisha kuwa, inawalinda na wale amba wanapanga kulipa kodi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu waajiri kutokulipa michango kwa wafanyakazi wao. Hili ni tatizo sugu na lazima tuhakikishe kuwa, wale waajiri wanalipa michango ipasavyo kwenye Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, nafikiri Mheshimiwa Waziri, atayazingatia na nitapata majibu muafaka wakati akifanya majumuisho. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zubeir, naomba nikushukuru kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, orodha ile ambayo imetosha kabisa kwa shughuli ya leo jioni imekamilika, lakini tumebakwa na wachangiaji takribani 11 na kwa kuwa mada yetu tutaihitimisha nadhani kesho jioni, kama *Order Paper* itatukubalia hivyo, basi huenda ikawa wachangiaji wale wote 11 waliobaki watapata nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwa hiyo, naomba waendelee kujiandaa na tutajitahidi waweze kupata nafasi hiyo kesho, ikwemo na wale amba walileta maombi yao kwa kuchelewa, lakini kwa kuzingatia michango yao katika Bunge hili, nadhani wanawenza kuwa na nafasi pia ya kuchangia hoja hii.

Sasa labda nikumbushe tu Kanuni Namba 53, ambayo inatulazimisha kutokuwahisha shughuli ambazo hazipo kwenye *Order Paper*, Kanuni Namba 53 (1) na (8), naomba tutakapokuwa tunaendelea na mchango huu tuendelee kulizingatia hilo. Kila mtu amekuwa na mshawasha mkubwa sana wa kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini tuwe na mipaka kama tulivyofanya leo, haikuwa mbaya sana lakini walitaka kuanza kuzama katika kuchangia Hotuba ya Rais, badala ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambayo ipo mbele yetu. Kwa hiyo, tutaendelea kuichangia kesho katika maeneo yanayogusa, lakini tuwe na mipaka kwa namna moja au nyingine.

Halafu wakati tunaendelea na michango hii, Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri utaiangalia katika kumbukumbu zako, wameomba angalau waelimishwe kwa kupatiwa semina maalum kuhusiana na masuala ya *stock exchange*, lakini hiyo unaweza ukaiangalia kwenye Wizara na kuona namna gani hilo linawezza likafanyika kwa faida pia ya wananchi wetu kule tunaowawakilisha.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunatoa michango yetu leo na hasa Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, aliomba mwongozo hapa. Naomba niendelee kusisitiza lile alilolisema yeze na alilolisema Mheshimiwa Ndugai na hasa baada ya kupata taarifa, nilichoona wakati nikifanya maamuzi ni kwamba, wote wanazungumzia hoja moja. Kama vile wanajenga hoja moja katika kuchukua miti, lakini kuelekeza katika ujenzi wa nyumba moja na Mheshimiwa Waziri ameendelea kusisitiza kwamba, mdahalo huo utakuwa na lengo la kuongeza kasi ya kuhamia Dodoma. Kwa hiyo, naomba niseme hilo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, pia ninalo tangazo lingine, Katibu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, washiriki kwenye Mkutano mkubwa sana kesho tarehe 26 Agosti, 2008 kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere na Mkutano huo unawaalika Waheshimiwa Wabunge, kushiriki katika Mkutano Maalum wa kuipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Rais, saa saba mchana. (*Makofî*)

Vilevile nina tangazo la mwisho na hilo linatoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Burudani, ninawaomba Wajumbe wa Kamati ile Ndogo ya Sherehe Bungeni, tukutane kwenye chumba cha Spika pale tunapotokea ili tuweze kubadilishana mawazo katika suala fulani mahususi kwa dakika mbili, tatu, kabla hatujatawanyika hapa.

Baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru na niwapongeze kwa shughuli zote za leo. Nawatakia jioni njema na niseme kwamba, naahirisha shughuli hizi mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi wa Bunge.

(*Saa 01.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 26 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)

